**Mwanafunzi** auawa kikatili, mwili wakutwa kwenye kichaka

UKURASA 2

**Vigogo** CHADEMA wachuana kwenye uchaguzi wa Kanda

UKURASA 3



**Naibu** Waziri aagiza uchunguzi ubadhirifu fedha za wanyamapori

UKURASA 5




# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Aprili 14, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581646

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**NGOZI LAINI**

UKURASA 14



RIPOTI MAALUM

# Kasi ongezeko 'single mothers' sasa yatisha

- **Kiini** chake chaanikwa, wataalamu wataja athari... *Ukurasa 4*

## Mpango ataka vijana wasikubali kugawanywa misingi ya itikadi

UK. 3




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikabidhiwa tuzo na Mwenyekiti wa Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Paul Kimiti, kwa ajili ya kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuliongoza taifa kwa mafanikio, wakati wa Maadhimisho ya Kitaifa ya Miaka 102 tangu kuzaliwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, yaliyofanyika jana katika Ukumbi wa Mikutano wa Jiji la Dodoma. **PICHA: OMR**



## Nchimbi ataka wanaoanguka waache nongwa

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YAPUNGUZWA KASI MBIO UBINGWA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Nchimbi ataka wanaoanguka waache nongwa

**Na Halfani Chusi,** MPANDA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ametaka viongozi wa chama hicho wanapoanguka katika nafasi za uongozi kutotafuta mchawi na kuacha kuwanunia walioshindwa bila sababu.

Pia amekemea kitendo cha baadhi ya viongozi wa chama hicho cha kuwadhalilisha watumishi wa umma pale wanapofuatilia utekelezaji wa ilani ya chama na kutengeneza mazingira ya kutaka fedha kinguvu.

Balozi Nchimbi alitoa kauli hiyo jana mjini hapa katika ziara ya viongozi wakuuu wa chama hicho inayohusisha mikoa sita, huku akisisitiza kuwa uongozi bora huanzia ngazi ya familia.

Katika ziara hiyo, kiongozi huyo ameambatana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makala, na Katibu wa NEC, Oganaizesheni, Issa Ussi Haji 'Gavu', ambao watafanya ziara katika mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya na Ruvuma. "Uongozi bora unaanzia ngazi ya familia, lakini wewe unatoka nyumbani kwako hakuna anayekuunga mkono, hujaongea na watoto wako halafu unataka uchaguliwe wewe. Mwisho wa siku utasikia familia yako wanasema huyu akishinda kazi tunayo. Lakini pia tabia ya kukataa matokeo tuiepuke kwa maslahi ya chama na serikali yetu.

"Hakuna mwenye akili asiyejua CCM ikipasuka nchi imepasuka. Ndiyo maana wapinzani baadhi wanatuambia, "jitahidi chama chenu kisipasuke" chama cha siasa madhubuti kinaongozwa na misingi ya kidemokrasia," alisema.

Balozi Nchimbi alisema kiongozi wa kweli ni yule anayekubali matokeo bila kusita na kujitolea mfano kuwa aligombea mara 28 na kuanguka mara nne.

"Nilipigwa kisawasawa lakini nilikubali matokeo. Wale mtakaoshinda mtumie nafasi hiyo kuwaunganisha wananchama na kufanya kazi pamoja na walioshindwa ili kushirikiana kuijenga nchi pamoja," alisema.

Nchimbi alisema mtu hawezi kuwa kiongozi kama ataanguka katika uchaguzi na kuamua kutuma wapelelezi kujua kama wanamwongelea vibaya.

"Huo si uongozi. Kuna wanachama ambao ni viongozi ndani ya CCM, wanalazimisha kupewa fedha na watumishi wa serikali, hao ni wezi kama wezi wengine tu, tunataka viongozi watende haki mtu akiulizwa haki inapatakana wapi, aseme inapatikana CCM. Ninaomba tuutimize wajibu huo bila kigugumizi," alisema.

Katika mkutano huo, Balozi Nchimbi aliwaahidi wananchi mkoani humo kushughulikia tatizo la umeme lililoibuliwa na Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Katavi, Idd Kimanta, ambalo limedumu kwa muda sasa.

Naye Makalla alisema katika ufanyaji wake wa kazi katika nafasi hiyo, hatoshughulikia migogoro ambayo kesi zake zipo mahakamani kwa kuwa, hicho ndicho chombo pekee cha kutoa haki.

"Hatuwezi kuiamrisha mahakama. Sisi tutawasaidia wananchi kwenye matatizo ambayo bado hayajafika mahakamani, lazima tuwe wa kweli, tuwaeleze wanachi, siyo kumwaaminisha kitu ambacho huwezi kumsaidia.

"Kuna mtu aliwahi kuja ofisini kwangu ameshindwa kesi katika mahakama zote halafu anataka mimi Mkuu wa Mkoa (wakati huo) ndio nitatue shida yake. Hilo haliwezekani nitakachoshauri labda akakate rufani.

"Mimi nitashughulikia migogoro ambayo bado haujafika mahakamani, kwenye kikao cha ndani tumepokea taarifa ya chama na serikali yapo mazuri yaliyofanywa na tumeridhishwa na utekelezaji wake," alisema Makalla.

Alisema wakati anaondoka Katavi, baadhi ya maeneo yalikuwa hayana lami, lakini ndani ya miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan yamewekwa.

"Ushuhudua mwingine Katavi ilikuwa inachukuliwa kama mkoa uliofungwa kwa sababu kulikuwa hamna barabara wala uwanja wa ndege lakini leo nimetua hapa kwa ndege.

"Kila mwanachama anapaswa kutembea akisimulia mambo mazuri yaliyofanywa, na wapo watu tukikaa bila kusema watasema serikali haijafanya chochote, mwambie ukitoka hapa mpaka Sikonge unateleza, Tabora unateleza mwambie kwa kujiamini kabisa," alisema Makalla.

Gavu aliwataka wanachama kutafuta viongozi wenye sifa wataokinadi chama hicho bila gharama na kuweza kushinda nafasi zote za uchaguzi.

"Tunahitaji kuwatumikia na kutumwa na mtu mwenye uthubutu na utayari, kama ni mwenyekiti ajue kilichompa thamani ni CCM. Wakati wa kukumbatia watu umepita. Tunahitaji mtu ambaye akisimama atakuwa nyenzo ya kutufikisha kwenye ushindi," alisema.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Balozi Dk, Emmanuel Nchimbi, akiwasili Mkoa wa Katavi jana na ujumbe wake kwa ajili ya kuanza ziara katika mikoa sita nchini. Katika ziara hizo ameongozana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makala, na Katibu wa NEC, Oganaizesheni, Issa Ussi Gavu. **PICHA: HALFANI CHUSI**

## Mwinyi awashukuru viongozi, wananchi dua kwa baba yake

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewashukuru wananchi na viongozi wa mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuendelea kumwombea dua na hitma baba yake mzazi, Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi, aliefariki dunia hivi karibuni.

Taarifa uiliyotolewa na Idara ya mawasilianio Ikulu, Zanzibar, alisema Dk. Mwinyi alitoa shukrani hizo juzi baada ya ibada ya sala ya Ijumaa iliyofuatiwa na visomo mbalimbali, hitima na dua kweye Msikiti wa Hidaya, Kilimani Tazari, mkoani humo.

Akizungumza kwa niaba ya familia yake, Dk. Mwinyi aliwashukuru wananchi hao kwa mapenzi yao kwa Mzee Mwinyi tangu walipomuuguza hadi alipofariki Februari 29, mwaka huu.

Naye Mkuu wa Mkoa huo, Rashid Hadid Rashid, alisema wanachi wa kijiji cha Kilimani Tazari na vijiji Jirani, kwa makusudi waliamua kukaa pamoja kumwombea dua Marehemu Mzee Ali Hassan Mwinyi, viongozi walio hai na wazee wa vijiji hivyo waliofariki dunia.

Akizungumza kwenye ibada hiyo, Sheikh Khamis Abdul Hamid aliwahusia waumini wa Kiislam kuendelea kufanya mema na kumcha Mwenyezi Mungu kwa haki ili roho zao zikawekwe mahala pema baada ya kufa.

Mapema, akikhutubu kabla ya sala ya Ijumaa, Khatib Sheikh, Omar Abdi aliwasihi wananchi na waumini wa dini ya Kiislam kuendelea kujenga hofu kwa Mwenyezi Mungu kwa kukithirisha ibada hata baada ya kumalizika kwa Mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Aliusia kwamba Mwenyezi Mungu hayuko Mwezi wa Ramadhan pekee bali siku zote, hivyo aliwanasihi waumini hao kuendeleza ibada kwa siku za kawaida kama ilivyokuwa Ramadhan.

Katika ibada hizo za visomo na dua na hitma pia waliombewa viongozi walioko serikalini, wastaafu, masheikh na wazee walio hai na waliotangulia mbele ya haki ndani na nje ya mkoa huo.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa dini na serikali akiwemo Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaab, na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja,

# Mwanafunzi auawa, mwili wakutwa kichakani

**Na Vitus Audax**

MWANAFUNZI wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Kilima, wilayani Bukoba, Elius Antony (13), anadaiwa kuuawa kwa kukatwa panga shingoni kisha mwili wake kutelekezwa kichakani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda, alisema uchunguzi wa tukio hilo bado unaendelea ili kubaini chanzo cha mauaji hayo.

Akisimulia tukio hilo, mama mzazi wa mtoto huyo, Beatrida Antony, alisema mara ya mwisho kijana huyo alikwenda na baba yake kuchoma mkaa porini, kisha alirudi nyumbani kufuata simu na Sh. 10,000 kwa ajili ya matumizi.

Alisema baba yake aliporejea alipokewa na salamu za pole kutoka kwa majirani kuhusu kupotea kwa mtoto.

"Baada ya muda mfupi alifika Mwenyekiti wa Kijiji na kumchukua baba yake na kumpeleka kichakani ambako mwili huo ulionekana ukiwa umejaa nzi," alisimulia.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kilimo, Izidory Kaiza, alisema Aprili 10, mwaka huu, alipokea taarifa za kupotea kwa mtoto huyo kutoka kwa wazazi wake ndipo ufuatiliaji ukaanza mara moja.

"Wakati tukiendelea kumtafuta tuliona nguo na mguu kichakani katika Kitongoji cha Mwizi na baadaye tukaona mwili mzima, hivyo tukawajulisha polisi ambao walifika na kuubeba kisha wazazi wakaitwa kwenda kuutambua,"alisema.

Alisema ilibainika kuwa mwanafunzi huyo alipigwa na panga shingoni na kuvuja damu hali iliyosababisha umauti.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kilima, Reginah Richard, alilaani kutokea kwa tukio hilo na kuwataka wazazi na walezi kuwa makini kwa kuwalinda watoto wao.

## HABARI KITAIFA




Vyombo vya usafiri vikipita kwa tabu katika shimo kubwa lililotuama maji kutokana na mvua za masika zilizoanza kunyesha katika eneo la Kitunda Kati jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mpango: Msikubali kugawanywa kwa itikadi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametaja maeneo manane ya kuzingatiwa na vijana ili kumuenzi Hayati Mwalimu Julius Nyerere likiwamo kutokukubali kugawanywa kwa misingi ya itikadi za kisiasa, dini, kabila au rangi na kuwataka wawe na umoja na mshikamano kwa maslahi ya taifa.

Akizungumza jana jijini hapa katika maadhimisho ya kumbukizi ya miaka 102 ya kuzaliwa Hayati Nyerere yaliyoandaliwa na Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dk. Mpango alisema vijana wana nafasi kubwa ya kudumisha amani.

Pia alisema wananafasi ya uhifadhi, matumizi endelevu ya rasilimali za taifa, utunzaji wa mazingira na historia ya ukombozi kusini mwa Afrika.

"Baba wa Taifa alitambua na kuhimiza kulinda amani katika taifa. Kupitia hotuba zake, Mwalimu Nyerere alitusisitiza Watanzania kuishi kwa amani na kuepuka ubaguzi kwa misingi ya rangi, dini, itikadi za kisiasa au kabila.

"Mwalimu alituasa kuwa na umoja na mshikamano ili kuweza kufanya kazi na kujiletea maendeleo. Serikali inaendelea kudumisha amani kwa kuendeleza misingi iliyowekwa na Baba wa Taifa,"alisema.

Dk. Mpango alisema Mwalimu Nyerere alianza harakati za kisiasa na ukombozi wa nchi akiwa kijana na zilizaa matunda ya kuwa na taifa huru.

"Katika serikali yake, Mwalimu aliwaamini viongozi vijana wanaume kwa wanawake na aliwateua kushika nafasi mbalimbali za uongozi," alisisitiza.

Kadhalika alisema katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, ni fursa kwa vijana wenye sifa kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

"Baba wa Taifa alisisitiza elimu kwa vijana katika kupambana na umaskini, vijana wa kitanzania mna nafasi kubwa ya kujiendeleza kielimu kwa manufaa ya taifa letu. Mtumie maarifa mtakayoyapata kutatua changamoto kwenye jamii yetu,"alisema.

Alisema takwimu za Sensa ya Watu na Makazi yam waka 2022 zinaonyesha kuwa asilimia 94 ya Watanzania wamezaliwa baada ya Muungano na asilimia 77.3 ya Watanzania ni vijana wenye umri wa chini ya miaka 35.

"Swali la kujiuliza hapa vijana wangapi mna uelewa wa kutosha kuhusu Muungano wetu? Je, mnatambua faida za Muungano na sababu za kuundwa Muungano? Vijana wote wa kitanzania kufanya jitihada za kuelewa misingi na faida za Muungano na kuwa mstari wa mbele katika kuulinda na kuuenzi Muungano wetu adhimu?" alihoji.

Dk. Mpango alisema serikali inaendelea kufanya juhudi mbalimbali za kutunza historia adhimu na mchango wa Tanzania katika ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika, na kuwaasa vijana wa kitanzania kuelewa kuwa, Tanzania ilishiriki ukombozi huo kwa kutambua kuwa, uhuru na usalama unategemea pia, uhuru wa nchi nyingine za Afrika.

Kadhalika, aliagiza Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuendelea kulinda, kutunza na kuhifadhi Malikale ikiwa ni pamoja na zilizokuwa nyumba na kambi za wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika hapa nchini.

"Aidha, Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere iangalie uwezekano wa kufanya kazi na wadau wengine, kuangalia namna bora ya kuhifadhi kumbukumbu za Baba wa Taifa kama inavyofanyika kwa waasisi wa mataifa mengine,"alisema.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dunstan Kitandula, alisema wizara imepata kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa makumbusho ya marais jijini Dodoma ambayo yatakuwa na eneo la kuonyesha historia ya Mwalimu Nyerere kitaifa na kimataifa.

Pia alisema eneo la ukombozi la Kongwa tayari limetangazwa kuwa urithi wa taifa kwa sasa.

Alisema alijipambanua kama kiongozi mzalendo kwa nchi na kutunga sheria kali dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali ya taifa.

Makamu wa Rais alizitaka mamlaka za uhifadhi zimuenzi kwa kuongeza jitihada za kutunza mazingira kwa ajili ya vizazi vijavyo.

**KIMITI: TUSIMSAHAU**

Mwenyekiti wa taasisi hiyo na mwanasiasa mkongwe, Paul Kimiti, alisema kuna namna ambayo watanzania wanamchukulia Nyerere kama mtu wa kawaida tofauti na anavyothaminiwa na mataifa mengine.

"Tunaendelea kumuenzi Baba wa Taifa, muendeleze fikra zake tumeona Wakatoliki wameanza kumuombea aitwe Mwenyeheri na baadaye Mtakatifu.

"Katika uongozi Mungu aliumba vidole vitano. Wafipa walikuwa wanasema vidole vitano vilikuwa vinabishana, Baba wa Taifa alisema, Mungu alikuwa na makusudi kuweka vidole vitano, kidole gumba ndio pekee kinakuangalia wewe usifanye lolote bila kushirikisha wenzako. Kiongozi hawezi kufanikiwa bila kutumia na viongozi wengine," alisema Kimiti.

**ALIFUNDISHA WATEULE**

Makamu Mwenyekiti Mstaafu wa CCM Tanzania Bara, Philip Mangula, alisema: "Alidai uhuru akiwa kijana mwenye miaka 32. Aliongoza nchi na alipofikia umri wa miaka 63, Aliomba kuacha na wengine waongoze. Sasa kwa umri ule alikubali kuacha mbwebwe zote, mshahara wa Rais akasema na mimi ninataka wenzangu waniongoze."

Mangula alisema katika uongozi wake (Nyerere) alihimiza umoja kwa kuwa, ndiyo nguvu ya watanzania na kutangaza Azimio la Arusha kuhusu namna ya kujenga nchi.

"Mwalimu akasema tunataka kutoa uamuzi wa kujenga nchi katika misingi ya ujamaa na kujitegemea, akajenga timu ya vijana ya kueneza uamuzi huu, sasa miongoni mwa vijana walioteuliwa ni Paul Kimiti tulikuwa vijana 75, mwingine anaitwa Philip Mangula,"alisema.

Alisema vijana hao walipelekwa jeshini na walipotoka akawaambia wao ni walimu wa siasa wafundishe siasa ya chama chao.

"Mwalimu alikuwa hana ubinafsi wa kupenda nafsi yake kuliko jamii. Sasa katika kazi tuliyoifanya mwenzangu Kimiti akawekwa Makao Makuu ya Chama Idara ya Elimu ya sias mimi nikapelekwa Kivukoni nimefundisha pale.

"Aliamini katika kufundisha sio umteue mtu ndiyo umpe kazi, sio kama jongoo unamwambia haya nenda, yeye aliamini ukimpa mtu kazi mfundishe mpe mafunzo ndiyo hayo mafunzo yalikuwa yanatolewa," alisema.

# Vigogo CHADEMA wachuana uchaguzi kanda

**Na Vitus Audax**

BAADHI ya wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wamejitosa kuchangisha fedha za wagombea kuchukua fomu za uchaguzi wa viongozi kanda, huku vigogo ndani ya chama hicho wakichuana kuongoza kanda hizo.

Siku mbili zilizopita CHADEMA kilifungua rasmi dirisha la kuchukua fomu kwa ajili ya uchaguzi wa viongozi wa kanda nne za kiutawala katika chama hicho.

Kwa mujibu wa Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Tanzania Bara, Benson Kigaila, mchakato wa kuchukua fomu ni endelevu mpaka Aprili 22, mwaka huu.

Wakati hayo yakijiri, uchaguzi huo umeonekana kuwa na ushindani mkubwa tofauti na miaka iliyopita kutokana na vigogo mbalimbali kutajwa kunyukana katika kanda zao, huku wengine wakiweka wazi nia zao mitandaoni.

Miongoni mwa vigogo wanaotajwa kuchuana katika kanda hizo ni pamoja na nafasi ya Mwenyekiti Kanda ya Victoria ni Mwenyekiti wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA) Taifa, John Pambalu, ambaye tayari ametangaza nia kupitia mtandao wake wa X na anatarajia kukabiliana na Hezekiah Wenje.

Wengine ni aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi Sugu' atakayechuana na Mchungaji Peter Msigwa anayetetea nafasi yake kwa Kanda ya Nyasa.

Kanda ya Magharibi mchuano ni baina ya Mawakili Dickson Matata na Peter Madeleka huku Kanda ya Serengeti ikitarajiwa kuwakutanisha Emmanuel Ntobi, John Heche, Lukas Ngoto na Gimbi Masaba.

Wakati mchuano ukiwa mkali kutokana na kuwapo vigogo hao, baadhi ya wana CHADEMA katika makundi sogozi mbalimbali ya chama hicho, wameonyesha kutembea kwenye nyayo za Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuanzisha 'mikeka' kuwachangia wagombea wanaowapenda ili kuchukua fomu.

Mmoja wa wachangishaji hao ni Machael Masele aliyeanzisha michango kwa ajili ya kumchangia fomu Wenje, ili agombee nafasi ya Mwenyekiti Kanda ya Victoria ambako mkeka huo hadi kufikia jana, ulikuwa na wachangiaji 29 huku Sh. 352,000 zikiwa zimechangwa. Licha ya mchango huo kuendeshwa katika makundi ya chama, kumeibuka hisia mbalimbali kwamba huenda ukakigawa kabla ya uchaguzi. Mchangiaji mmoja, Kapalatu Masanja, alitolea mfano kwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi.

"Kesho wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi Tanzania nao wanakuja na mahaba kwa Rais Samia Suluhu Hassan, wanamchangia fomu pia ni wapigakura na ni wasimamizi wa kura yaani sipati picha (akimaanisha katika makundi hayo wapo wajumbe, wasimamizi pamoja na wapigakura)," alisema. Lackson Mjuni, alisema utaratibu huo hauna tofauti na alichokiita 'uchawa' (kujipendekeza) na kuhoji kuwa hali hiyo haina tofauti na upande wa watu wa CCM kuwa kiongozi anayehitaji nafasi hawezi kukosa fedha ya kuchukulia fomu.

Hata hivyo, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Zakaria Obad, aliingilia mjadala huo na kusema suala hilo si kosa na yeyote anaweza kufanya hivyo kutokana na kukutanishwa na siasa.

"Mashabiki wana haki ya kushindanisha mtu wao ili mradi wasiende nje ya katiba, kanuni na miongozo ya chama hususani miongozo wa taratibu za kuendesha kampeni za uchaguzi ndani ya chama toleo la 2012," alisisitiza.

Aidha, alitoa wito kwa wanachama hao kuchukua fomu kwa kuwa dirisha bado liko wazi na kila mwanachama ana haki ya kuchukua kwa mujibu wa katiba na kanuni za chama hicho.

RIPOTI MAALUMU

# Kasi ongezeko 'single mothers' yatisha

**Na Jenifer Gilla**



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima.

"SITAKI mwanamume wa kunimiliki na sina shida ya ndoa. Kama ni mtoto ninaye sasa ndoa ya nini?

Ilikuwa kauli ya mwanadada mmoja akiwa na wenzake watatu katika mapumziko ya jioni sehemu ya starehe baada ya saa za kazi, pengine wakisubiri muda kupungua kwa msongamano wa magari ili warejee nyumbani. Kauli hiyo ilipokewa kwa vicheko na wenzake ambao walionekana kukubaliana naye.

Kimtazamo, wanadada hao walionekana kuwa ni watu wenye uwezo kutokana na hali zao. Kundi hilo ni kiwakilishi tu cha kinadada na kinamama wengi ambao hawataki ndoa na wengi wao wameshazaa ama mtoto mmoja au wawili na wana uwezo wa kuwalea na kuwatunza bila msaada wa baba zao. Miongoni mwao ni ni mameneja, wakurugenzi katika taasisi au wafanyabiashara.

Hivyo ndivyo hali ilivyo kwa kinamama hao ambao wanalea Watoto wenyewe, maarufu kama 'single mothers' na ongezeko la kundi hilo kwa sasa linakua kwa kasi nchini. Madada na wamama hao wenye ukwasi wanachagiza ongezeko hilo, mbali na wale waliofiwa au kuachwa na waume zao.

Utafiti uliofanywa na ICF Macro mwaka 2011 unaonyesha kuwa nchini Tanzania, asilimia 19 ya watoto wanalelewa na mama pekee na asilimia tano wanalelewa na baba wakati ripoti iliyofanyika mwaka 2016 inaonyesha kuwa idadi ya kinamama wanaolea watoto ni asilimia 38.

Mfanyabiashara wa nguo Kariakoo, Salma Rashid, anasimulia kuwa baada ya kuachana na mwenza wake akiwa na mtoto wa miezi sita, alimzuia kabisa kuwahudumia kwa chochote kwa sababu anajiweza.

Anasema mwanamume huyo aliwasumbua kwa muda mrefu kutaka kuhudumia mtoto wake na alivyoona usumbufu unazidi, alibadilisha namba ya simu na kuhama eneo walikokuwa wanaishi na sasa anaishi kwa amani na mtoto wake.

"Sihitaji chochote kutoka kwake. Kama tumeamua kuachana kila mtu afanye mambo yake. Nina uwezo wa kulea na kusomesha mtoto wangu sina shida na chochote kutoka kwake," anasema Salma.

Jamila Abdallah anasema haoni haja ya kusumbuana na mwanamume kuhusu malezi ya mtoto wakati Mungu amempa uwezo na kumlea mwenyewe.

Anasema kitendo cha kumpigia mzazi mwenzake kumkumbusha majukumu na ulezi wa mtoto ni kujishushia heshima kwa mtu ambaye hastahili, ikizingatiwa kuwa alimwacha na maumivu makubwa.

Mama mwingine, Cecilia Bernard, anasema anafurahi kuona mwanamke analea mtoto wake mwenyewe kwa kuwa inamjengea heshima na kuondoa dharau mbele ya mwanamume.

"Unajua ukiwa unalelewa mtoto na mwanaume ambaye mmeshaachana anakudharau. Kwanza, unakuwa unamnyenyekea tu yeye maana ndiye anakusomeshea mwanao. Mimi ninayapitia hayo kwa sasa na ikitokea siku nikapata pesa, mwanangu nalea mwenyewe," anasema.

Wakati wanawake hao wanaona ni vyema kukaa na kuwalea watoto bila msaada wa baba zao, Salum Abdallah anasema kitendo cha kukataa kushirikiana kulea watoto na wenza wao kisa wameachana si kizuri kwa kuwa kinamnyima baba haki ya kulea watoto. Anasema kitendo hicho pia kinawafanya watoto kukosa malezi ya baba.

Anasema wanawake wa aina hii wengi wao hawataki kabisa baba na mtoto wawasiliane, wakidhani kuwa wao pekee wanatosha kulea kumbe kila mzazi ana nafasi na umuhimu wake katika makuzi ya mtoto.

**TAKWIMU ZA TALAKA**

Talaka na kutengana kwa wanandoa ni moja ya sababu za ongezeko la kinamama hao. Takwimu za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) zinaonyesha kuwa mwaka 2019 talaka zilikuwa 442, mwaka 2020 zilifikia 511 na mwaka 2021 ziliongezeka hadi kufikia 550.

Aidha, takwimu za migogoro ya ndoa zilizotolewa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum zinaonyesha kulikuwa na migogoro 39,571 kwa kipindi cha Julai 2021 na mpaka Aprili, 2022 migogoro 19,262 ilipata suluhu, 15,718 bado ilikuwa katika usuluhishi na 4,576 mahakamani.

**WASEMAVYO WATAALAM**

Mwanasaikolojiatiba, Dk. Saldeen Kimangale, anasema chimbuko la suala hilo ni kuwapo kampeni za kumwinua na kumwonyesha mwanamke kuwa anaweza, hivyo kusababisha hali ya kujiamini kuwa kubwa kiasi cha kutoona umuhimu wa mwanamume katika maisha yake.

Anasema pamoja na kuwa kuna ushahidi wa kutosha kuwa mtoto kulelewa na mzazi mmoja hakuna madhara, bado kuna ushahidi mwingi pia unaoonyesha kuwa mtoto aliyelelewa na mzazi mmoja, hasa mama, anakabiliwa na changamoto za kihisia na kitabia.

"Watoto waliolelewa na mzazi mmoja, hasa mama kwa sababu ya kutengana, ugomvi au kukomoana tu kama ilivyozoeleka, leo hii wanakabiliwa na tatizo kubwa la hasira za haraka, ugomvi wa mara kwa mara, kuharibu vitu au kupoteza, kukosa umakini na kujiingiza kwenye tabia hatarishi kama vile kutumia vilevi," anasema.

Msaikolojiatiba Isack Lema anataja sababu nyingine kuwa ni uwapo wa taarifa nyingi mbaya zinazohusu uhusiano ambazo husambaa mitandaoni kama vile wanawake kuuawa na wenza wao, kupigwa na kusambazwa na kuwatia hofu wanawake kuendelea na uhusiano. Kutokana na matukio hayo, anasema wanawake wengi wanakuwa hawana mpango wa kuishi na wanaume kwa kuhofia kudhuriwa na unapofika umri wa kutaka Watoto, huamua kutafuta wanaume wa kuzaa nao tu kisha kutoweka na watoto.

Anasema wakati mwingine husababishwa na migogoro ya ndani na kufanya wanawake kupata sonona na kupungua hamu ya kujamiiana. Hali hiyo husababisha uhusiano kuvunjika na mama kuamua kulea mtoto mwenyewe.



Mama akiwa na Watoto. Kasi ya kinamama wanaolea watoto wenyewe inaongezeka kila uchao. **PICHA: MAKTABA**

Lema anataja pia uwapo wa hamasa kutoka kwa wanawake wenzao ikiwamo makundi yanayojiita 'single mothers' kwa kutiana moyo kuwa wanaweza na wengine hujifunza kutoka kwa mama zao.

**KASISI ALONGA**

Padre wa Kanisa Anglikana Mtaa wa Mikaeli na Malaika Wote, Tabata jijini Dar es Salaam, Joseph Upio, anasema suala hilo si sawa kwa sababu vitabu vya dini vinakataza wanandoa kuachana na mama kulea mtoto mwenyewe ingawa kuna wakati migogoro hutokea na kusababaisha hali hiyo kutokea.

Anasema ni wajibu wa wazazi wote wawili kuwalea watoto hao ili wakue vizuri kiroho jambo ambalo ni vigumu kutekelezeka kwa mzazi mmoja kwa kuwa mtoto anajifunza kwa wazazi wote wawili.

**NINI KIFANYIKE?**

Dk. Saldeen anashauri wazazi kabla hawajaamua kuzaa, watafute wenza wenye mienendo inayofaa ili wawatafutie watoto mama au baba bora.

"Tenga muda wa kutosha kujua historia ya makuzi ya huyo unayekwenda kumposa au anayekuja kukuposa. Kama kuna maharibiko yoyote katika historia ya utoto wake, tambua kuwa yumo kwenye vihatarishi," anasema.

Pia anawashauri wanawake wanaolea watoto wenyewe, waache kukimbia, kujificha au kupambana wenyewe ili kuonyesha jamii kuwa wako imara wakati ukweli ni kwamba wanatokota na kuyeyuka ndani kwa ndani.

Badala yake, anasema watafute tiba na kisha wafanye juhudi wapate wenza sahihi, hata ikibidi warudiane na wenza wao baada ya kujifunza na kurekebisha makosa na dosari zao ili wawape watoto nafasi ya kufurahia utoto wao wakiwa na wazazi wote wawili.

Lema kwa upande wake, anashauri jamii kufundisha mabinti namna kuanzisha na kuishi kwenye uhusiano wenye afya, ikiwamo kuwauliza wenza wao maswali ya msingi yatakayowapa majibu ya kule wanapoelekea.

Pia anasema wale waliotoka kweye uhusiano ambao si salama, watafute msaada wa kisaikolojia kabla ya kuingia kwenye uhusiano mpya ili kuondoa mawazo chanya kwa kuwa si kila aliyeachika hajaolewa.

Padre Upio anasema ni jukumu la vyombo vyote vya dini kutilia mkazo katika maadili ya kidini ili kusiwapo ndoa zinazovunjika na wazazi wote wawasaidie watoto kukua kiroho.

HABARI KITAIFA

# Mwenge warejesha matumaini ya maji

**Na Mashaka Mgeta,** LUSHOTO

DHANA ya Mwenge wa Uhuru kuleta matumaini pasipo na matumaini, upendo pasipo na upendo, na heshima palipo chuki na dharau, umethibitika katika kijiji cha Magamba Coast, kata ya Magamba wilaya ya Lushoto mkoani Tanga.

Baada ya kufika jana kwenye kijiji hicho chenye vitongoji vinane, mahali palipojengwa tangi, wakazi wa eneo hilo walipaza sauti zao wakisema, licha ya tangi la Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuwapo kwenye eneo lao, mtawanyiko wa maji unakwenda maeneo mengine pasipo kuwafikia.

Taarifa za wananchi hao zilimfikia Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024, Godfrey Mnzava, ambaye baada ya kuipokea taarifa ya RUWASA Wilaya ya Lushoto, alikwenda kulikagua tangi hilo.

Akiwa katika ukaguzi huo, Mnzava akabaini kwamba wananchi wa Magamba Coast, wamepoteza matumaini kuhusu kupata maji kupitia tangi lililoko kwenye kijiji chao, ndipo akampigia simu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso.

Wakati huo, Mnzava alikuwa na Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Japhari Kubecha, mbele ya wananchi hao wakionekana kusubiri kauli yenye kuibua matumaini kwao kupata maji moja kwa moja kutoka kwenye tangi hilo.

Simu ya kwanza ikapigwa na Mnzava kwa Aweso, aliyemthibitishia kwamba serikali inatambua kwamba wananchi hao hawapati maji ya moja kwa moja kutoka kweye tangi hilo ndiyo maana imeweka mpango madhubuti wa kuwaondoa kwenye kadhia hiyo.

Mnzava aliporejea kutoa tamko baada ya kuutembelea mradi huo, alisema Mwenge wa Uhuru umeridhishwa na maendelezo yake, kisha akawaeleza wananchi kuhusu mazungumzo yake na Aweso kwa njia simu.

Pamoja na maelezo hayo, Mnzava alisema ni busara na kwa vile Aweso yupo, atoe tamko kwa wananchi hao kwa njia ya simu ili Mwenge wa Uhuru wenye ujumbe usemao 'Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu' uweke kumbukumbu katika ufuatiliaji wake.

Ndipo watu walipotulia pale Aweso alipoanza kuzungumza akisema ni dhamira, nia na utashi wa Rais Dk Samia Suluhu Hassan kuwaondoa wananchi wote kwenye kadhia ya ukosefu wa maji na kwamba maagizo aliyoyapokea kutoka Mwenge wa Uhuru 2024 ni kwamba wakazi wa Magamba Coast watapata maji moja kwa moja kutoka kwenye tangi lililoko kijijini kwao.

Alimwagiza Meneja wa RUWASA Mkoa wa Tanga, Mhandisi Upendo Lugongo na mwenzake wa wilaya ya Lushoto, Mhandisi Erwin Sizinga, kuhakikisha wakati Mwenge wa Uhuru ukiondoka mkoani Tanga, siku inayofuata mkandarasi akabidhiwe eneo la kusambaza mabomba kwa ajili ya huduma ya maji kuwafikia wananchi hao.

Kauli ya Aweso iliibua shangwe kubwa kwa maelfu ya wananachi wa rika tofauti walioupokea Mwenge wa Uhuru kijijini hapo, wengine wakipunga matawi ya miti, vitambaa na kanga kama ishara ya kuupokea ujumbe huo kwa shangwe,

Mnzava pia alimwelekeza Kubecha kuhakikisha kuwa maagizo ya weso yanatekelezwa, na kwamba kabla ya kwenda eneo la mradi, mkandarasi mhusika akutane na Mkuu wa Wilaya huyo na taarifa zake kutolewa kwa Mwenge wa Uhuru.

Awali, taarifa ya RUWASA ilieleza kuwa mradi huo unaogharimu takribani Sh. bilioni mbili na utekelezaji wake kufikia asilimia 70, utawahudumia watu 30,835 wanaoishi kwenye maeneo ya Magamba, Kwesimu, Bara, Jegestal, Kambinambanne, Chakechake, Kitivo, Maguzoni, Sinza, Lushoto Mjini, Mabwawani, Kipembe na Kialilo.



Mwendesha Baiskeli ya miguu mitatu (Guta), akiwa amepakia mzigo mkubwa wa madumu akipita barabara ya Kawawa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Samia ateua tena

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemteua Balozi Said Othman Yakub kuwa Balozi wa Tanzania nchini Comoro.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Balozi Yakub anachukua nafasi ya Balozi Pereira Silima ambaye amemaliza muda wake.

Pia juzi, Rais Samia alimteua CPA Anthony Kasore kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

"Kabla ya uteuzi huu, CPA Kasore alikuwa akikaimu nafasi hiyo,' ilisema taarifa hiyo.

Rais pia alimteua Goodluck Shirima kuwa Kamishna wa Petroli na Gesi, Wizara ya Nishati. Shirima kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mkuu wa Kitengo cha Sheria na Uhusiano wa Kampuni ya Mafuta ya Puma Energy Tanzania.

Rais Samia tangu aingie madarakani miaka mitatu iliyopita, amekuwa akifanya uteuzi na utenguzi mara kwa mara ikiwa ni sehemu ya kuimarisha serikali ili kuendana na kasi anayoitaka.

# Taasisi yafungua mfumo mpya uendeshaji shule

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI inayojihusisha na mifumo ya kidijitali katika uendeshaji wa shule nchini (ShuleSoft), imezindua toleo jipya la mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa shule za msingi na sekondari kidijitali baada ya ule wa zamani kudukuliwa.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam katika uzinduzi wa toleo jipya la mfumo huo, Mkurugenzi wa ShuleSoft, Ephraim Swilla, alisema wamefanya maboresho ya mfumo kuongezea baadhi ya vipengele ambavyo havikuwapo awali kutokana na mapendekezo ya wateja na kudhibiti wadukuzi. Alisema mfumo mpya wa ShuleSoft unajihusisha na usimamizi wa shule, kusaidia masuala ya utawala, taaluma, kifedha, mawasiliano na kurahisisha ujifunzaji kwa mfumo wa kidigitali.

Swilla aliongeza kuwa toleo jipya limeunganisha wadau mbalimbali zikiwamo benki na mitandao ya simu kwa ajili ya malipo shuleni na kuokoa muda kwa utawala, wazazi na wanafunzi. "Mfumo wa toleo hilo jipya la ShuleSoft unakwenda kusaidia masuala ya usimamizi wa shule katika nyanja mbalimbali ambazo ni mahudhurio, maktaba, bweni, taaluma, mawasiliano ya moja kwa moja na wazazi pamoja na uwajibikaji wa wafanyakazi. "Shule sasa inaweza kusimamia mambo ya mahudhurio, maktaba, bweni lakini tunacho kipengele cha kutuma mawasiliano kwa wazazi. Tumeuunganisha na WhatsApp, Telegram ikiwamo program tumishi (aplikesheni) mpya ya simu inayoitwa (ShuleSoft parent experience) ambapo mzazi atajua kila kitu kinachoendelea shuleni.

Aidha, Swilla alitoa onyo kwa watu wanaoiba kazi za wabunifu na kufanya udanganyifu kwa shule na kuharibu ubunifu uliofanyika kwa kutumia jina la taasisi hiyo na kutengeneza taswira mbaya kwa jamii kwa kujiingizia kipato kwa njia ya udanganyifu.

Mwanasheria wa ShuleSoft, Faraja Msuya, aliwaonya watu wanaotumia nembo ya taasisi hiyo kufanya udanganyifu na kwa atakayebainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Tayari mfumo huo umezinufaisha shule za msingi na sekondari 470 nchini na kufungua ofisi katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mbeya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Aliyoyasema Rais Samia kuhusu Sokoine liwe somo kwa viongozi

**JUZI,** taifa liliadhimisha kumbukizi ya miaka 40 tangu aliyekuwa Waziri mkuu, Edward Sokoine alipofariki dunia. Hafla ya kumbukumbu hiyo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi, ilifanyika nyumbani kwa kiongozi huyo shujaa, aliyetumikia taifa kwa uaminifu, Monduli Juu mkoani Arusha.

Katika hafla hiyo iliyohudhuriwa pia na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, viongozi waandamizi wa serikali, dini na wastaafu pamoja na familia ya Sokoine, Rais Samia aliwataka viongozi serikalini kusimamia maagizo wanayopewa bila kutetereka na kuiga uthubutu wa kiongozi huyo.

Rais Samia alisisitiza kwamba wateule wake hao wanapaswa kutekeleza majukumu yao bila kuyumbishwa na shinikizo kutoka kwa mtu au kikundi cha watu bali wasimame katika misingi na kutenda haki. Alisema somo ambalo Watanzania hususani viongozi wanalipata kutoka kwa Hayati Sokoine ni kuwajibika kama alivyokuwa akifanya kwa kuwa alisimamia misingi ya haki na mienendo na matendo yake yalionyesha mfano bora wa uongozi.

Katika kuiga mfano huo, Rais Samia alisisitiza kuwa viongozi wanapaswa kusimamia uamuzi unaotolewa na serikali kuhusu jambo lolote na kwamba ukishatolewa (uamuzi), kinachofuata ni utekelezaji tu, hivyo viongozi lazima wafanye hivyo kama ilivyoafikiwa bila kuyumbishwa na ikiwezekana wawe mfano kwa wengine.

Rais Samia aliwakumbusha viongozi na watanzania kwa ujumla kuwa Hayati Sokoine alikuwa mpenda maendeleo kutokana na nyakati tofauti kusisitiza watu kufanya kazi huku akichukia uvivu, uzembe na watu kujilimbikiza mali. Sokoine katika uhai wake alipambana na uhujumu uchumi, biashara za magendo na ulanguzi kiasi cha kuchukiwa na watu waliokuwa wakijihusisha na vitendo hivyo.

Kutokana na tabia na hulka hiyo, alisema licha ya kwamba ni miaka 40 tangu alipoaga dunia, Sokoine bado anaishi kutokana na matendo yake na ni mfano wa kuigwa katika uongozi. Pia alibainisha kuwa serikali yake inafuata nyayo zake katika kuwaletea maendeleo wananchi kwa kupeleka huduma mbalimbali kama afya, elimu, maji na miundombinu.

Kuna msemo kwamba huchukua miaka mingi, hata karne, kupatikana kwa mtu mwenye haiba, hulka na tabia ya mtu aliyesimama katika nafasi fulani ikiwamo ya uongozi na alikuwa mfano katika jamii husika. Ndivyo ilivyo kwa Sokoine ambaye ni vigumu kupatikana mtu wa aina yake katika matendo na mwenendo kwenye uongozi.

Sokoine alipambana na dhuluma, uzembe, uvivu na umangimeza na aliwataka viongozi kutenda haki pamoja na kusimamia na kutekeleza yale wanayokubaliana. Hakuwa na simile hata kidogo dhidi ya mtu aliyeshindwa kutekeleza majukumu yake. Alikuwa mtu wa kuthubutu na mfuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na serikali.


Kutokana na tabia yake hiyo, aliwahi kusimama kidete na kumtaka naibu waziri mmoja afukuzwe kwa kushindwa kutekeleza maagizo aliyopewa. Sokoine alimwambia aliyekuwa Rais wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, kuwa alikuwa tayari kujiuzulu iwapo naibu Waziri huyo asingefukuzwa. Nyerere alikubaliana naye na hatimaye kumfukuza.

Kwa mfano huo tu, inaonyesha alikuwa mtu wa namna gani katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli mbalimbali hasa maagizo yaliyotolewa kwa viongozi kutoka kwa walio juu yao. Hali hiyo ni tofauti na sasa kwani wako baadhi ya viongozi katika ngazi mbalimbali hawatekelezi majukumu yao na hata kufanya kazi kwa mazoea.

Hayo yamebainika wakati wa ziara za Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na viongozi wa juu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika maeneo mbalimbali ambako hukutana na vilio vya wananchi kuhusu kutotatuliwa matatizo yao na viongozi wanaomwakilisha Rais huko. Hatua hiyo imesababisha mara kadhaa Rais kuwatumbua au kufanya utenguzi wa wateule hao. Hiyo ni dalili kwamba watu hao hawatimizi wajibu wao.

Kama alivyosema Rais Samia kwamba uthubutu wa Sokoine linapaswa kuwa darasa kwa viongozi wa sasa kwenye nafasi zao, ni vyema kila mtu akatekeleza wajibu wake kwa kusimamia na kufuatilia masuala mbalimbali kwa lengo la kuipaisha Tanzania katika viwango vya juu kimaendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mikoa hii inusuru vijana dhidi ya janga la uvutaji bhangi

**MIKOA** ya Mara, Morogoro, Arusha, Pwani, Kagera na Mwanza, imetajwa kuwa vinara wa kilimo cha bhangi, ambacho kinasababisha baadhi ya vijana kutumia kilevi hicho na kuhatarisha afya zao

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitaja mikoa hiyo hivi karibuni wakati akizindua Mbio za Mwenge wa Uhuru, mjini Moshi Kilimanjaro, na kusema serikali itawachukulia hatua za kisheria wote wanaolima zao hilo.

Kwa mujibu wa Majaliwa, kumeibuka aina nyingine ya bhangi, amnbayo ina kiasi kikubwa cha kilevi kiitwacho cha Arusha na Skanka, na kwamba aina hiyo ya bhangi ina sumu nyingi.

Lakini jambo la kusikitisha, anasema vijana wanaotumia bhangi hiyo, wanafahamu hicho kitu cha Arusha na Skanka, wengi wa waraibu ni watoto, vijana wenye umri wa miaka 13 hadi 24.

Kwa maelezo hayo ya Waziri Mkuu, ni wazi kuna haja ya kuchukua hatua ambazo zitasaidia kunusuru vijana wadogo ambao wanajihusisha na uvutaji bhangi na kuhatarisha afya na maisha yao ya baadaye.

Ikumbukwe kuwa, vijana ndio wanaotegemewa kuwa nguvukazi na taifa la kesho, wakiachwa waendelee kuvuta bhangi, inawezekana siku za usoni taufa likawa na vichaa wengi wanaotokana na kilevi hicho.

Hivyo, ninadhani hatua ya kwanza inayopaswa kuchukuliwa, ni vijana wenyewe kujitambua na kuacha bhangi, elimu itolewe kuhusu madhara yake, lakini pia wakulima wa bhangi wakuchuliwe hatua za kisheria.

Njia hizo zinaweza kusaidia kuokoa maisha ya vijana ambao wameingia kwenye janga hilo la kuwa vichaa na wale ambao wana mpango wa kutumia kilevi hicho wakidhani kuwa huo ndio ujana.

Inasikitisha kusikia kuwa vijana wa miaka 13 hadi 24 wenye umri wa kuwa shuleni au vyuoni, ambao bado wana safari ndefu wa maisha, wanavuta bhangi bila kujali kwamba inaweza kukatisha ndoto zao.

Mwaka 2022, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa na Uhalifu liliripoti kuwa takriban watu milioni 192 duniani, wa kati ya umri wa miaka 15 na 64 wanatumia bangi kwa burudani, kulingana na takwimu za 2018.

Katika ufafanuzi wake, shirika hilo likasema kuwa, karibu asilimia 35 ya watumiaji hawa wana umri wa kati ya miaka 18 na 25, ambao kimsingi bado vijana wenye safari ndefu ya kutafuta maisha.

Hao ni vijana, ambao akili zao bado zinaendelea kukua, na kwamba uvutaji wa bhangi unaweza kuwafanya wakapata athari zaidi katika ubongo kutokana na matumizi ya muda mrefu ya bhangi.

Suala la kilimo cha bangi limekuwa la mjadala wa muda mrefu kutoka kwa watu wa kada mbalimbali wakiwamo wabunge ambao baadhi yao wamewahi kushauri kujengwa kwa viwanda ambavyo vitapunguza makali yake ili kutumika kwenye maeneo mbalimbali.

Hoja mojawapo ya kutaka kuhalalisha zao hilo ikiwa ni kwamba, wapo baadhi ya watu ambao wakitumia bhangi, wanaweza kupata nguvu za kufanya kazi zaidi, ikiwamo kulima.

Pamoja na jitihada zaa kutaka kuifanya bhangi kutimiwa hadharani baada ya kuondolewa makali, ninadhani nguvu kuwa ielekezwe kuwanusuru vijana kwa kuwazuia kuitumia.

Bangi, cocaine, heroin na mirungi, vyote hivyo ni miongoni dawa ya kulevya zenye madhara kwa afya ya binadamn, hivyo ni vyema kunusuru kizazi kijacho badala ya kushauri jinsi ya kupunguza makali.

Wataalam wa afya wanasema, watumiaji wengi wa dawa za kulevya ikiwamo bhangi, afya zao huathirika, moyo kwenda mbio sivyo kawaida, kinywa kukauka, macho kuwa mekundu na kutokuwa na hamu ya kula.

Kwa hiyo mikoa inayojihusisha na kilimo cha zao hilo, ijitajahidi kuachana na kilimo hicho, ili kunusuru vijana dhidi ya janga la uvutaji bhangi ambalo limetajwa na Waziri Mkuu.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Buriani Zephania Ubwani, mwandishi wa wito aliyeifia habari hadi mwisho



Pascal Mayalla

JUMATATU iliyopita, Aprili 8, ilikuwa siku ya kuzaliwa kwangu. Nilipoingia kwenye kundi sogozi la WhatsApp la Jukwaa la Wahariri, nikakutana na taarifa iliyotumwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa TEF, Anita Mendoza.

TEF imetuma salamu za rambirambi baada ya kutokea kifo cha mwandishi wa habari mkongwe nchini, Zephania Ubwani, kilichotokea Aprili 6, 2024 wakati akitekeleza majukumu yake ya kazi.

"Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), limepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha mwandishi Zephania Ubwani kilichotokea tarehe 6 Aprili, 2024. Kifo cha Ubwani ambaye alikuwa mwandishi wa gazeti la The Citizen linalochapishwa na Kampuni ya Mwananchi Communications Limited (MCL), kilitokea ghafla.

"Taarifa za awali zinaeleza Ubwani alianza kupata tatizo la afya wakati akifanya mahojiano na Mkurugenzi wa COSTECH (Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia) katika hoteli ya Kibo Palace, jijini Arusha. Alijisikia vibaya na kukimbizwa katika Hospitali ya AICC ambako alifariki dunia wakati akifanyiwa uchunguzi.

"Hata hivyo, uchunguzi wa daktari umeeleza kuwa Ubwani alikuwa na tatizo la moyo kwa muda mrefu ,hivyo alipatwa na shambulio la moyo. Jukwaa la Wahariri Tanzania tunatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, Chama cha Wanahabari Arusha na Mwananchi Communications Ltd kutokana na msiba huo," ilisema taarifa hiyo iliyotowa saini na wa na Deodatus Balile, Mwenyekiti wa TEF.

Baadaye nikasoma taarifa nyingine ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) makao makuu, Arusha, nayo ikiadhimisha maisha ya Ubwani, mwandishi wa habari wa Tanzania mwenye tajriba ya zaidi ya miongo mitatu.

Ubwani alitumia sehemu nzuri ya kazi yake ya kupongezwa akishughulikia mchakato wa mtangamano wa EAC. Alikuwa mwanahabari mashuhuri akifungua na kusimulia hadithi ya EAC kwa mamilioni ya watu wa Afrika Mashariki na nje ya Afrika kupitia habari na makala katika magazeti ya The Citizen na Mwananchi na machapisho mengine mengi dada chini ya Nation Media Group katika Afrika Mashariki.

Akiwa mmoja wa wanahabari wazoefu waliowahi kuandika habari za EAC, Ubwani aliandika kwa lugha rahisi na ya kutamka ambayo iliwavutia watu mbalimbali waliofahamiana na maandishi yake.

Hakuna aliyeiambia EAC hadithi bora kuliko Ubwani ambaye pia alishauri na kuwafunza waandishi wengi wajao kuripoti kuhusu EAC na masuala mengine muhimu kikanda na kimataifa.

Ubwani alikuwa amepitia mafunzo kuhusu mtangamano wa EAC kupitia warsha mbalimbali za mafunzo ya vyombo vya habari zilizoitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo alielewa vizuri mchakato wa ujumuishaji, mwanzo wake, mafanikio na changamoto.

Pia alikuwa kiongozi mchapakazi na mnyenyekevu aliyeacha alama kwa wote waliotangamana naye. Mara kwa mara alikuwa akitembelea makao makuu ya EAC kukutana na uongozi na wafanyakazi ili kujulishwa maendeleo katika jumuiya nzima.

Ubwani alijulikana sana katika korido za mashirika na taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kama mwandishi wa habari ambaye angeweza kuwasaidia kutangaza habari kuhusu mchakato wa mtangamano wa Afrika Mashariki. Kazi yake bora katika kuripoti habari, namna ya kidiplomasia na mchango mkubwa katika juhudi za mtangamano wa kikanda wa EAC itakuwa mioyoni mwetu milele.

Japo nilifahamia na Zephania Ubwani kupitia maandishi yake mengi akiwa Daily News wakati kukiwa na Zephania Musendo (naye marehemu Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi), hivyo nikawa nawachanganya sijui yupi ni yupi. Musendo alipopata changamoto fulani ndipo sasa nikamfahamu Zephania Ubwani.

Nilifanya nao kazi za kihabari kila nikiwa Arusha na siku moja kukatokea tukio fulani jijini humo ndipo urafiki wetu ukashikamanishwa na zege, tukawa chanda na pete.

Baadhi ya waandishi wa Arusha ni mafia wa zile bahasha za waandishi! Nilikuwa na kazi ya kihabari ya mkutano wa kimataifa wa siku tatu katika hoteli ya Ngurdoto, nikaalika waandishi kutoka vyombo vya habari, mwenyeji wangu alikuwa na uwezo wa kuwahudumia waandishi 20 tu, hivyo nikaalika idadi hiyo, nikawaambia wajitegemee nauli. Nikawa muwazi kuwaeleza unene wa bahasha zao, kumbe kosa! Waandishi wa Arusha wakaambiana, wakajialika, kuja kuhesabu wamefika waandishi zaidi ya 40!

Mimi niliwakomalia kuwa nitawalipa wale tu niliowaalika, waliojialika wajibebe na kupambana na hali zao. Ili kuzuia nisizongwe, nikawapandisha kwenye usafiri wa pamoja bahasha zao nitawatumia kwa 'mobile money'.

Walipoondoka wakasemezana, Pasco ametubagua, ametukosea sana, waandishi wa Arusha tuna mshikamamano, hakuna kutoa story ya mkutano huo! Taarifa za kufanyiwa mkomo baridi zikanifikia, waandishi pekee waliosimama na mimi ni Ubwani, Daily News, Uhuru na TBC na RTD, wengine wote wakapiga mgomo baridi wa mshikamano. Zephania akasema hawa waandishi watoto, wao wanaangalia tu bahasha, stori kubwa hii huwezi kuifanyia mgomo kwa sababu tu ya bahasha, akaniandikia stori nzuri ya Kiingereza na Kiswahili na kunipatia, nikawatumia wahariri wenyewe, kwenye TV nikasambaza mwenyewe, hivyo story ikatoka kwenye TV zote na kesho yake kwenye magazeti japo si yote!

Ubwani alithamini kazi na si pesa mpaka siku ya umauti. Alikuwa kwenye tukio, hivyo hiyu ni mwandishi, aliyeupenda uandishi hadi kuufia. Ukisikia uandishi wa wito ndio huu.

Buriani Zephania Ubwani kwa kuufia uandishi akiwa na umri wa miaka 71 na bado alikwenda kwenye 'beat'.

**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mavieite na bendera za chama vitatuponza



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HIVI karibuni matukio ya ukamataji wahamiaji haramu nchini ndiyo yamekuwa Waingereza wanaita 'The talk of the town', Waswahili wakatafsiri kuwa ni 'habari ya mjini'.

Yaani tangu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, ahadharishe kuhusu watu hao wanaojiopenyeza nchini na kutaka hatua zichukuliwe, inaonekana wahusika wanasema "mtatufanya nini!"

Majuzi tu, Jeshi la Polisi Mkoa wa Manyara, lilikamata gari 'vieite' zamani tukiyaita mashangingi, likiwa limebandikwa namba inayoonekana kuwa na serikali; STL 1964 likiwa na wahamiaji 17 kutoka Ethiopia.

Gari hilo ambalo namba zake zilikuwa kumbe za magumashi, lilikamatwa katika kijiji cha Kiongozi wilayani Babati, kumbe namba zake halisi tukaambiwa na wahusika kuwa ni T 723 BSF.

Kabla ya tukio hilo, kumbe Machi 23 kukawa kumekamatwa vieite lingine likiwa na wahamiaji 20 katika kizuizi cha Minjingu wilayani Babati pia katika mkoa huo huo!

Hili lilitia fora, kwani lilikuwa likipeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), likiwa na namba T 774 BDL likiendeshwa na dereva aitwaye Edward Erihard wa Dodoma, dogo tu mwenye umri wa miaka 31.

Wambea hawakukaa kimya walipoona bendera ya CCM wakatazama na namba za gari, wakafukunyua na kubaini kuwa kumbe mmiliki wake ni kada wa CCM na anaishai Ilala, Dar es Salaam. Siwezi kumtaja bila ushahidi.

Wakati tunafuatilia kujua hatima ya hao waliokamatwa Manyara mara tunasikia tena Aprili 8, mwaka huu huu tulionao, tena kipindi cha Mfungo, wanakamatwa wahamiaji wengine haramu 16 katika msitu wa Luganga, Sao Hill, Mufindi.

Wanavyopenda maviete sasa, hawa safari hii wakiwa katika vieite lenye namba za Serikali kama kawa, ambazo ni STL 3999 tunazoambiwa nazo ni za magumashi, kumbe halali ni T 803 CVW eti mmiliki wake ni Said Hassan wa Tabata!

Kama vile haitoshi, Februari 20 mwaka huu huu, vieite lingine likadakwa katika Kijiji cha Mazinde, Korogwe mkoani Tanga likiwa na namba T 888 CEA likiwa nao 16. Wote hao wanatoka Ethiopia wakiwa njiani kwenda Afrika Kusini.

Kabla sijaenda mbali bila shaka mimi na wewe tunaweza kujiuliza, hawa jamaa zetu ni wahamiaji au wakimbizi kutoka huko uhabeshini, na wamekamatwa Manyara, Iringa na Tanga, tena kwenye magari ya nguvu kama hayo, yanayotumiwa mara nyingi kama si na matajiri basi na wanaojiita waheshimiwa.

Kwa kifupi, ni magari yanayotumiwa na wabunge na mawaziri kama si wakuu wa mikoa na wilaya, wanaotaka tuwaheshimu na kuwaita waheshimiwa, huku sisi wakituita sijui kina nani au labda tusioheshimiwa na ndiyo sababu hawaheshimu sheria kwa sababu zinaheshimiwa nasi.

Hivi kwa akili ya kawaida tu, inakuwaje mtu atoke Ethiopia mpaka aingie nchini hadi katikati mwa nchi asikamatwe basi angalau Kenya, basi Namanga au Horohoro kama si Sirari? Ina maana kote huko hakuna polisi hakuna maofisa Uhamiaji?

Ina maana askari na maofisa wanaochukia tabia hii ya uhamiaji haramu wako Manyara, Tanga na Iringa peke yake? Na kwa nini mavieite tu na namba za serikali na bendera za CCM ndizo zitumike kupitisha kiharamu Waafrika wenzetu hawa?

Hivi nikipendekeza wanapokamatwa wasiwekwe ndani wala kufunguliwa mashitaka na badala yake ama waruhusiwe kwenda waendako huko Kwa Mandela au warejeshwe kwao watotako nitakuwa nimekosea nini?

Sikatai, mhamiaji haramu anakiuka sheria za uhamiaji halali na hastahili kuchukuliwa vyovyote zaidi ya kuadhibiwa, lakini adhabu ya kukaa nao magerezani wakitumia kidogo tulichonacho ni kujichosha kiakili na kimwili, bora wasiwepo.

Na ili kuhakikisha hawapo, ni kuwasindikiza tu waendako ili wakapambane na wenye nchi hayo huko, huku nasi tukibaki na wahamiaji halali wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Rwanda na Burundi kama tulivyozoea.

Lakini kubwa; kubwa ni kwamba kwa nini watumie namba za serikali kwenye magari yao? Kwa nini bendera za CCM kwenye magari yao? Ni rahisi tu jibu lake; ni kwamba hawakamatwi na wala hawakumbani na kizuizi chochote njiani.

Kwa kuwa tumeshazoea kuwa viongozi wa serikali na chama tawala 'hawavunji' sheria, basi mwavuli wanaotumia wasafirishaji wa wahamiaji haramu na mihadarati, unawasaidia kufikia malengo yao, kwani wakamatwao ni wasioheshimiwa tu.

Inawezekanaje mtu aingie nchini, avuke mikoa yote hiyo mpaka akamatwe katikati ya nchi? Ina maana kwamba humo njiani hana kizuizi na askari wakiona STL au Bendera ya CCM wanapisha njia. Apite mwenye namba ya raia au bendera ya upinzani! Weee thubutu!

Sasa kama kweli tuko makini na nchi yetu, basi kila gari linalohisiwa jinai lisipite kwa gia ya namba za Serikali au bendera ya CCM, hapo ndipo tutaweza kulinda usalama wa nchi, vinginevyo magaidi wataingia kwa namba hizo na bendera hizo hizo. Niko paleee!

## Wasisitiza kudumisha upendo na mshikamano

**Na Jumbe Ismailly** SINGIDA

WAUMINI wa dini ya Kiislamu mkoani Singida wamehimizwa kuendelea kudumisha amani, umoja, upendo na mshikamano waliokuwa nao wakati wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kupiga vita mmomonyoko wa maadili.

Naibu Amiri wa Jumuiya ya Answari Suni Tanzania (JASUTA) Mkoa wa Singida, Sheikh Abdurahmani Hassan, alitoa wito huo kwenye hotuba aliyotoa kwenye swala ya Eid Elfitri iliyoswaliwa kwenye Kituo cha Mafunzo ya Korani cha mjini Singida.

Alisema katika kipindi cha mfungo wa Ramadhani, waumini wote walikuwa katika hali ya amani na utulivu na karibu watu wote walishaungana na kuwa na nyoyo za ukarimu na kusaidiana.

"Kuhusiana na hali tuliyokuwa nayo kwa mwezi wa Ramadhani tulikuwa katika hali ya amani na utulivu sana na watu wote karibu walishaungana wamekuwa na nyoyo za karibu na kusaidiana hivyo tunaomba Mwenyezi Mungu ajaalie lakini pia tunausiana tuendeleze hiyo hali, "alisisitiza.

Kwa mujibu wa Naibu Amiri huyo, kuna mmomonyoko wa maadili takribani nchi nzima hususani kwa upande wa vijana kutokana na kundi hilo kutokubaliana na wanayoambiwa na wazee kwa kuwa wanajiendesha kupitia simu zao.

Kuhusu faida za kutoa wakati lifitri na wanaopaswa kutoa zaka hiyo, Amiri wa JASUTA Mkoa wa Singida, Sheikh Yahya Mohamed, aliwataja kuwa ni waumini wa Kiislamu waliokuwa wamefunga swaumu ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Hata hivyo, alisema wanaostahili kutoa zaka tilifitri kwanza ni wale waliofunga mwezi wa Ramadhani kuashiria kwamba wao ni waislamu na wameitika wito huo na wakawa na umiliki wa kitu kinachotolewa zaidi ya matumizi ya kawaida.

"Tafsiri yake, ,mtu ameweza kununua nguo za watoto wake amelipa kodi, amelipa umeme, amelipa maji lakini na mahitaji muhimu ya siku hii Eid na kesho kinachobaki ndicho kinachopaswa kukitolea katika zaka tilifitri," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Kituo cha Mafunzo ya Korani cha Al-Furqaan Singida, Mohamed Abrahaman Mohamed, alitumia fursa hiyo kwa kuwakumbusha wazazi na walezi kuwaandalia watoto wao mazingira mazuri na yatakayowasaidia kwa siku za baadaye badala ya kuwaachia mali na fedha nyingi.

# Waziri aagiza uchunguzi ubadhirifu fedha vijiji mradi wa wanyamapori

**Na Munir Shemweta,** MLELE

MBUNGE wa Kavuu na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amemwomba Mkuu wa Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, Alhaji Majid Mwanga, kuunda kamati ya kupitia mapato na matumizi ya fedha za Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) katika Halmashauri ya Mpimbwe ili kubaini kama kuna ubadhilifu ili wahusika wachukuliwe hatua.

Pia amemwomba mkuu huyo wa wilaya kuchunguza Sh. milioni 44 zilizotolewa na mkandarasi anayejenga barabara ya Kibaoni hadi Sitalike, zinazodaiwa kulipwa kwa kijiji bila kufuata utaratibu.

Pinda alisema hayo juzi kwa kwa nyakati tofauti wakati wa mikutano yake ya hadhara na wananchi wa vijiji vya Mirumba, Ilalangulu na Kibaoni katika Halmashauri ya Mpimbwe, wilayani hapa.

Alisema hayo baada ya kubadilishwa uongozi wa WMA ndani ya mwezi mmoja tu ambapo kamati ilifanikiwa kukusanya Sh. milioni 200 tofauti na kamati iliyokaa kwa zaidi ya miaka 10 na kudaiwa kutosaidia maendeleo yoyote ya vijiji husika. "Iundwe tume ya kupita kitabu kwa kitabu tujue miaka 20 fedha zetu ziliend a wapi za wananchi hao. Wiki mbili Sh. milioni 200, hebu tuwaulize miaka 20 wameleta nini?" alihoji Pinda.

"Pia kuna ubadhilifu wa Sh. milioni 44 zilizotolewa na mkandarasi anayejenga barabara ya Kiabaoni-Sitalike ambaye amelipa kwa kijiji bila utaratibu. Uchunguzi nani amechukua fedha taslimu ambazo hazijulikani zilipokwenda wapi ufanyike," alisisitiza.

Pinda alisema mpango wa WMA una faida kubwa kwa vijiji vinavozunguka hifadhi na kutolea mfano wa wilaya ya Tanganyika inayonufaika. Kwa mujibu wa Pinda, mwaka huu vijiji vinavyozunguka hifadhi vitapokea Sh. bilioni 16 .

Alisema kiasi chochote cha fedha kitakachopatikana kupitia WMA lazima wananchi wahusishwe matumizi yake ili fedha zinazokusanywa zitumike kwenye shughuli za maendeleo ya vijiji husika.

Alhaji Mwanga aliahidi kuunda haraka timu itakayohusisha vyombo vya ulinzi na usalama kama vile Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Jeshi la Polisi na Magereza ili kubaini kama kuna ubadhilifu wowote wa fedha za umma. Alisema iwapo itabainika hivyo, wahusika watachukuliwa hatua stahiki.

"Hakuna atakayepona katika suala hilo na lazima tutawashughulikia wahusika wote watakaobainika kuwaibia wananchi. Kazi hii tunaiweza na hatutacheka na mtu hata mmoja," alisema.

Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Jamii (WMA) katika Halmashauri ya Mpimbwe, wilayani ya Mlele, inahusisha vijiji vya Kibaoni, Mirumba, Ilalangula na kijiji kimoja kutoka wilaya ya Nkasi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Dk. Selemani Jafo (katikati), akizungumza na Watendaji wa Ofisi hiyo wakati wa utambulisho wa Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto), na Naibu Katibu Mkuu (Muungano). Abdallah Mitawi (kulia), wakati wa kumkaribisha Mhandisi Luhemeja mara baada ya kuwasili katika ofisi ndogo za Ofisi ya Makamu wa Rais zilizopo Jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujitambulisha kwa Viongozi na Watendaji kufuatia uhamisho wake kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu) hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC akemea watendaji kuwatosa wananchi

**Na Steven William** MUHEZA

MKUU wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Zainabu Abdallah, amekemea tabia ya watendaji wa serikali kukaa ofisini badala ya kwenda kwa wananchi kutatua kero zinazowakabili.

Amesema watendaji hao wanapaswa kubadilika na kutekeleza kwa vitendo majukumu yao kwa kuwafuata wananchi waliko na kusikiliza kero zikiwamo migogoro ya ardhi.

Abdallah alisema hayo juzi wakati akisikiliza kero za wananchi katika uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti wilayani hapa ijulikanayo 'Soma na Mti' iliyofanyika katika Shule za sekondari za Potwe na Kwabastola kata ya Makole. Takribani miti 4,000 ilipandwa kupitia kampeni hiyo.

Watendaji wa serikali, alisema lazima waende kwa wananchi kusikiliza kero ikiwamo migogoro ya ardhi na kuzitatua badala ya kumsubiri mkuu wa wilaya aende kwa wananchi.

Alisema mtendaji yeyote wa serikali katika idara yake ambaye atashindwa kwenda kusilikiliza malalamiko ya wananchi na kuyatatua basi ahame katika wilaya hiyo.B"Wewe mtendaji ni lazime utoke uende kwenye maeneo ukaangalie ni jinsi gani unaweza kusuluhisha migogoro ya jamii na wawekezaji," alisema.

Pia alisema dhamira ya serikali ni kuleta wawekezaji nchini waishi vizuri na wananchi wa wilaya yaa Muheza na si kuanzisha migogoro ya ardhi.

"Rais Samia (Suluhu Hassan) ameifungua nchi kwa uwekezaji, amekwenda nchi mbalimbali duniani kutangaza fursa za uwekezaji tulizo nazo hapa nchini na amewaita wawekezaji wamekuja nchini kuwekeza. Sasa kukiwa na migogoro na wananchi, itakwamisha juhudi za Rais," alisema.

"Wawekezaji tunawapenda waje kuwekeza nchini lakini nao wananchi wana nafasi yao. Wanalima mashamba, wanapanda mazao yao ili kusomesha Watoto. Sasa mkiwafukuza kwa ajili ya kumpa mwekezaji ardhi ndio inaleta migogoro. Hiyo sitaki katika wilaya hii," alisema.

Alisema baadhi ya watendaji wa serikali katika halmashauri wanatoa ardhi ya wananchi kwa wawekezaji kwa maslahi yao na kusababisha migogoro mikubwa kitu ambacho si kizuri.

Mkuu wa wilaya alisema wiki iliyopita alikwenda katika kijiji cha Kambai, kata ya Kwezitu, ambako kumetokea mgogoro wa ardhi ya mashamba kati ya wanachi na mwekezaji, hivyo kusababisha kutokea fujo jambo ambalo si zuri.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa wilaya aliwataka vijana kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.

Aliwahamasisha vijana na wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo ili kuleta mabadiliko katika jamii.

Nichukue nafasi hii kuwahamasisha mama zangu, dada zangu pamoja na vijana kujitokeza kwa wingi kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa pindi mchakato utakapotangazwa rasmi," alisema.


# MAISHA

APRILI 14, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*






## MWENDO WA POCHI

Ukurasa 13

# WATOTO


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | | S | I | M | B | A |
| B | | | | B | | S |
| I | | M | I | A | | H |
| N | A | E | | T | I | I |
| G | | Z | A | A | | N |
| W | | W | | | | D |
| A | M | A | N | I | | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


GOA, GIA, NOA, ANA, ELIMU, MWAGA, DIMBA, GANZI, NIPASHE, ANGALIA

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI


MSAIDIE RAFIKI YAKO KULIFIKIA UA



## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na ragiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukumuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mchawi hajasinzia usiku na mchana kwa miaka 30!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na ushuhuda wa mchawi mmoja aliyeamua kujilipua hadharani na kutoa siri zote. Baadaye akaokoka kwenye kongamano la injili lililoongozwa na Mchungaji Ezekiel kutoka Kenya kwenye uwanja wa Biafra, Kinondoni DSM, Machi 22, mwaka huu.

Ushuhuda huu nilianza kuutoa wiki iliyopita kwa wale waliosoma safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo, kwenye NIPASHE hii kila Jumapili. Hakika ni Mwanga wa Jamii.

Alielezea jinsi alivyoshirikishwa katika uchawi ambao alisema pia ukoo wao ulikuwa ni wachawi wakubwa. Akataja baadhi ya silaha wanazotumia kufanya ushetani huo kuwa ni pamoja na Simba, chatu, nyuki, vyura na fisi.

Akaelezea mambo ya kichawi aliyofanya katika maisha yake hadi kupelekea kukatwa mguu baada ya kukiuka masharti kwa wakuu wake wa kichawi. Baada ya ulemavu huo akakimbilia kuokoka. Hebu msikie anavyoeleza mwenyewe.

Baada ya kuwa mlemavu nikaokoka. Walokole wakaja kuniombea nyumbani kwangu wale wanyama Simba, chatu, fisi wakawa havionekani, walipotea lakini bado vitu viwili vikawa vinanisumbua. Vyura bado vimo ndani na hawa nyuki walihama kwangu wakahamia kwenye kiwanja changu kingine.

> **"Akasema ana watoto wa kike wanne warembo sana. Lakini hakuna mwanaume aliyekosea hata namba aje awaoe. Niliua sana mimi.**

Lakini ile nyumba ya milango minne ipo bado sijaivunja. Lakini nikiwa nimelala usiku, huwa napigwa na yule chatu. Ananitoa kitandani ananitupa chini kisha anatoweka. Kwa hiyo bado hiyo roho inanisumbua. Ninafunga sana, ninaomba sana na kutoa sadaka, lakini bado huyo roho mchafu amenizidi nguvu.

Mchungaji Ezekiel akamkatisha na kumwambia, "ni kwa sababu ulikataa kutoa sadaka ya mke, baba, mama au mtoto. Tena wakitaka watakutoa huu mguu mwingine. Wewe ni kiongozi wa wachawi na unaasi na madhabahu ya uchawi haijavunjwa ndio maana chatu anakuja anafanya kazi yake.

Siku ile simba atakuja atakumaliza kabisa. Wakiwa wanataka wakupige, wakuadhibu, wanatuma ugonjwa ili ukatwe mguu. Kwa sababu wewe haustahili kukatwa mguu wala mimi Ezekiel siwezi kukatwa mguu sababu niko katika ufalme wetu. Ndio maana nasimama tangu saa saba ni giza tu limeingia.

Sababu natumika katika ufalme wetu, badala ya mimi kukatwa mguu nawasaidie wale wanaolemaa, wanapata nguvu wanaendelea.

Ezekiel anaendelea kusema: "Ukiona nyoka ndani ya samaki, fahamu ameasi madhabahu yake. Sasa wakati unapigwa mguu ulikataa kutoa sadaka, wanaweka ugonjwa kwako ili utoe."

Sasa ile kwamba nyoka anakuchapa kofi unaanguka chini, siku wakiamua kuja simba wanaweza kukufanya jambo lolote. Mtoa shuhuda akakiri ni kweli na kusema; Nyoka anapokuja hujiviringisha mguuni na kumtupa chini.

Halafu kuna kipindi mbuzi beberu wanakuja wawili, mwekundu na mweupe wanagombana. Wameshikana vichwa, lakini huyo mwekundu anakuja kwangu, huku mweupe anamsukuma mwenzie ili waje wanigonge. Wakishanikaribia tu usingizi unaisha.

Nina miaka 30 sijasinzia usiku wala mchana. Sijapata usingizi hata dakika tano! Nimewahi kuoa wanawake 15 na ninao watoto 21. Mke wangu wa mwisho huyu hapa ni wa 16, wengine wote 15 walishaondoka kwangu.

Mke huyu wa 16 alipohojiwa na Mchungaji Ezekiel alisema ana watoto sita na mumewe huyo. Hao wanawake walioondoka walikuwa wakiishi na bwana huyu miaka mitatu wanaondoka. Baba huyu anasema alizaliwa mwaka 1961 na huyu mke wa mwisho umri wake miaka 43.

Akasema ana watoto wa kike wanne warembo sana. Lakini hakuna mwanaume aliyekosea hata namba aje awaoe.

Niliua sana mimi.

Msomaji wangu, kipengele hiki cha kuua sana fuatilia wiki ijayo mambo mazito sana. Aliua watu wa aina gani na kwa njia zipi, usikose uhondo huo japo wa kusikitisha katika safu hii.

Bila shaka msomaji wangu umeanza kupata picha mambo yanayofanyika katika ulimwengu wa giza unaotawaliwa na shetani. Wapo watu wanaojikuta wakifanya mambo mabaya pasipo wao kutaka kama baba huyu. Hakupenda mambo ya kichawi lakini akalazimishwa. Na hata alipojaribu kukataa alikumbana na adhabu kali kama alivyopigwa na nyoka na pia kukatwa mguu.

Wapo watu waliowatoa kafara wanafamilia, baba, mama, watoto kwa udanganyifu wa shetani ili kupata na mali nyingi. Hata hivyo, watu wa aina hii wameishia pabaya sana. Kazi ya ibilisi ni kuua, kuharibu na kuchinja.

***Tafuta nguvu ya Mungu mpendwa kudhibiti wachawi. Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Wafanyabiashara mtajificha kwenye hicho kichaka hadi lini?

WATANZANIA walio wengi wamekuwa wakitumia muda wao mwingi kufikiria kuhusu fedha, hatua ambayo imewafanya muda wote kushikwa na wasiwasi inakuwaje wakikosa.

Jambo hilo linawaumiza kichwa kwa sababu hawana fedha ya kutosha, hasa wakati wanapokweenda dukani au sokoni na wanapokutana na bei za vitu wanavyovitaka viko juu.

Serikali nayo inatumia muda mwingi kufikiria kuhusu fedha hiyo hiyo kwa madhumuni tofauti na baadhi ya watu wanavyofikiria.

Rais Samia Suluhu Hassan naye amenukiliwa akisema: "Nilipomwapisha Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), nilimwambia nenda kakusanye kodi. Tunazihitaji kwa ajili ya maendeleo lakini kodi za dhuluma hapana.

"Nilisema hivyo kwa kutambua serikali inahitaji mapato yatokanayo na kodi ili kutimiza majukumu yake, ikiwamo kuhakikisha wananchi wanapata huduma za kijamii. "Nilisisitiza haki kwenye ukusanyaji wa kodi nikiamini kwenye dhuluma baraka za Mungu hazipo. Leo miaka mitatu baadaye napenda kusisitiza msimamo wangu wa kutokukubaliana na kodi za dhuluma.

"Nafarijika tangu tulipoanza kusisitiza ukusanyaji wa kodi kwa haki, makusanyo yanaendelea kuongezeka; kwa mfano makusanyo yamependa kutoka Sh. trilioni 18 mwaka 2021 hadi Sh. trilioni 24 mwaka 2022."

Jambo muhimu kwa jamii nyingi ni kuwa na maisha mazuri au kuongeza kipato kwa kadiri inavyowezekana.

Unaweza kujiuliza pato halisi ni kitu gani, jibu ni uwezo wa kujipatia bidhaa na huduma kwa mtu mmoja mmoja. Sasa nyie mnaokwepa kulipa kodi mtajificha hadi lini?

Bei za mahitaji kama chakula, nishati na malazi, ni miongoni mwa vinavyopanda kwa kasi kuliko vingine. Hivyo makundi ya watu wenye kipato cha chini hutumia kiasi kikubwa cha fedha wanachopata kwa ajili mahitaji hayo kuliko wale wenye kipato kikubwa.

Fedha ni njia tunayoitumia kununua mahitaji kwa matumizi yetu. Katika dunia ya sasa, uamuzi mbalimbali katika masuala ya kiuchumi, umekuwa ukifanyika kwa kutumia fedha.

Fedha hiyo imekuwa na nguvu katika manunuzi ya bidhaa na utoaji wa huduma hiyo ndio sababu noti na sarafu zimetambulika moja kwa moja kama fedha.

Kama tunatumia kiasi kikubwa cha fedha kununua mavazi, hii ina maana kuwa viwanda vya nguo vitakuwa kwa wingi.

Hata hivyo, kabla hatujatafakari suala la kodi, ni vyema tukafahamu kuhusu kupanda na kushuka kwa bei za bidhaa; hii inatokana na wengi wetu kupata wasiwasi pindi bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinapoanda kila kukicha, huku kilio kikubwa kikiwaendea watu wenye vipato vya chini.

Kupanda kwa bidhaa na huduma husababisha kuporomoka kwa hali za maisha, ambapo itampasa mtu kununua bidhaa kidogo na kupata huduma kidogo kuliko ilivyokuwa kabla ya kupanda kwa bei.

Kwa mujibu wa Kanzidata ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), mfumuko wa bei wa taifa kwa kipimo cha mwaka, unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi.

Mfumuko wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia Mei, 2023 umefika asilimia 4.0 kutoka asilimia 4.3 kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2023.

Hii inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Mei, 2023 imepungua ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2023.

Fahirisi za bei zimeongezeka kutoka 108.42 mwezi Mei, 2022 hadi 112.72 mwezi Mei, 2023. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2022/2023, TRA ilivuka lengo la kukusanya hadi kufikia Sh. trilioni 24.76 kutoka Sh. trilioni 24.11 za mwaka wa fedha uliopita.

Makusanyo hayo ya nusu mwaka ni ongezeko la asilimia 11.5 ikilinganishwa na makusanyo ya Sh12.49 trilioni yaliyofikiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha uliopita, 2022/23.

Ndiyo maana nasema tunapaswa kulitazama kundi hili lenye kipato cha chini ambalo mara kadhaa matumizi yao yamekuwa makubwa kuliko kile wanachokipata au tuseme hakilingani ili kukamilisha mahitaji yao kama chakula, malazi na mavazi.

**•Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI




Ni tukio la kukumbukwa na Gloria Samson Paulo wakati familia yake ilipomfanyia sherehe ya aina yake ya kumuaga iliyofanyika Oktoba 28, 2022 katika ukumbi wa Cavilam barabara ya Iringa Jijini Dodoma.

MITINDO

Na Moshi Lusonzo








# MWENDO WA POCHI

POCHI ya mkononi kwa wanawake ina umuhimu katika kukamilisha suala zima la uvaaji.

Inaelezwa pochi za mkononi hutoa mwonekano maridadi kwa mwanamke hasa anapotoka katika matembezi ya jioni.

Haijalishi aina gani ya mavazi waliyovaa, lakini pochi inaweza kubadilisha mtazamo na kuwa wa kuvutia zaidi kwa mwanamke.

Hata hivyo, jambo la kuzingatia hapa ni rangi ya pochi kama inafanana na mavazi husika, ili kuondoa uwezekano wa kuharibika kimwonekano.

Kuna baadhi ya mambo ambayo yanahitaji kuzingatiwa wakati wa kununua mfuko kwa wanawake.

**Rangi ya pochi**

Rangi inapaswa kuendana na mavazi uliyovaa wakati huo. Wanawake wengi kwa kawaida hupendelea kununua mikoba ya rangi nyeusi kwa sababu huendana na nguo nyingi.

Kwa upande mwingine, ikiwa utanunua pochi yenye rangi kali, basi nguo iwe na rangi iliyopooza. Kama vazi lako lina rangi ya kung'aaa, ni vizuri ukabeba pochi yenye rangi hafifu.

**Idadi ya vyumba:**

Unashauriwa kuwa na mkoba wenye vyumba zaidi ya kimoja kwa ajili ya kukurahisishia kubeba vifaa vyako kama vipodozi.

Pia unapaswa kuwa na uwezo wa kuchukua chochote unachohitaji haraka.

Ukubwa wake

Pochi ndogo inayobebwa nyakati za jioni hautakiwi kuwa na ukubwa kupita kiasi, inatakiwa kuwa ya kawaida ambayo ni rahisi kuibeba mkononi.

UREMBO

Na Mary Geofrey



# Ngozi laini

NGOZI laini na haina kasoro humuongezea ujasiri na kujiamini kwa mwanamke.

Wanawake wengi wanapenda kuwa na ngozi nyororo na yenye afya, lakini bado wana uelewa mdogo wa namna ya kutengeneza ngozi kuwa katika hali hiyo.

Katika safu ya leo tutaelezana namna ya kutumia asali kuongeza umaridadi wa ngozi ya uso.

**Kulainisha ngozi**

Mtu mwenye ngozi kavu, asali inasaidia kulainisha ngozi na ina tabia ya kuvuta unyevu kutoka kwenye hewa na kuhifadhi.

Unachotakiwa chukua asali mbichi kijiko kimoja cha chai kisha paka usoni, halafu kaa nayo kwa dakika 15 hadi 20 kisha safisha uso wako.

**Kusafisha ngozi**

Katika kusafisha ngozi asali ina uwezo wa kuua bakteria na kuvuta uchafu katika matundu ya ngozi na kutoa nje, hivyo inasaidia pia kuondoa tatizo la chunusi.

Hapa unatakiwa kuchukua asali mbichi kijiko kimoja cha chakula, changanya na mafuta ya nazi vijiko viwili na kisha paka usoni huku ukisugua taratibu kwa kuzungusha vidole.

Ukimaliza kusugua uso na mchanganyiko wako, osha uso wako na maji ya vuguvugu.

**Kusugua ngozi**

Ukitaka kusugua ngozi chukua kijiko kimoja cha asali na kijiko kimoja cha baking soda.

Tumia mchanganyiko huu kusugua ngozi yako taratibu. Asali inaongeza lishe na chembe chembe kuzuia madhara yanayotokana na sumu za hewani zinazozeesha ngozi.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mihogo na Chachandu



MIHOGO ya kukaanga ni chakula pendwa hasa ile inayokaangwa na wafanyabiashara wadogo wa mitaani.

Watu wengi wanavutiwa na aina hii ya chakula, lakini baadhi hushindwa kupata kutokana na kuhofia mazingira na wakati mwingine kutokana na hadhi yao ya kimaisha.

Leo nakupa njia nzuri ya namna ya kukaanga mihogo kwa ajili ya chakula maalumu cha familia yumbani kwako.

**Maandalizi**

Mihogo mikubwa mitatu, mafuta lita moja, kitunguu kimoja, kitunguu swaum kiasi, tangawizi kiasi, nyanya nne, limao moja, karoti nusu, hoho nusu, pilipili manga kidogo, chumvi na pilipili mbichi.

**Jinsi ya kuandaa**

Menya mihogo, ikatekate katika vipande unavyotaka na kisha isafishe.

Bandika karai ya kukaangia, weka mafuta na mihogo ndani, weka maji kidogo na funika na mfuniko unaozuia mvuke kutoka.

Mihogo ikianza kuchemka punguza moto ili iive taratibu na kulainika vizuri hadi maji uliyochanganya na mafuta yakauke.

Kisha funua, utaona mihogo yako ikiwa imeiva vyema, anza kutoa mmoja mmoja ile ambayo imeiva na kuanza kukauka vyema, tayari kwa ajili ya kuliwa na kachumbari ama chachandu.

**Chachandu**

Osha nyanya, karoti, hoho, tangawizi, chukua sufuria uvisage uvitie, kisha katakata kitunguu tia, twanga pilipili uitie pia. Weka chumvi na pilipili Manga.

Bandika jikoni uweke na maji nusu kikombe na unyunyuzie mafuta kiasi. Funika acha ichemke dakika tano, kisha kamulia limau uache ichemke kidogo, epua chachandu yetu itakuwa tayari kwa kuliwa na mihogo.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Using'ang'anie mwonekano wa zamani wa nyumba yako



BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha mwonekano.

Mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa.

Si vibaya kufanya hivyo lakini hata pale bajeti inapokuwa ndogo unaweza kufanya maboresho hayo.

Miongoni mwa vitu ambavyo unaweza kuvitumia kubadilisha mwonekano wa nyumba yako hata bila kutumia gharama kubwa na ikapendeza ni pamoja na namna kuchagua rangi ya ukuta.

Nyingine ni matumizi tofauti ya karatasi za ukutani na malighafi zingine zilizotumika kutengenezea samani zako ambazo zikitumiwa vizuri zina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa muonekano wa nyumba yako na kukupa wa kuvutia zaidi.

Kwa mfano kupaka rangi upya kabati la luninga, miguu ya kiti au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa, kunasaidia kubadilisha muonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili vitu kidogodogo kama vile vigae na fimbo za pazia, mapazia yenyewe, zuria na mapambo ya ukutani.

Viko vitu vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke.

Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo. Kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na zilizoko kwa wakati wa sasa.

Kama vitu vyako vya ndani umevitumia kwa miaka mingi na vimepitwa na wakati na ndiyo maana huenda vinakuchosha na kuiona nyumba yako mbaya, usiikatie tamaa kwa sababu inawezekana kuirudisha katika ubora wake. Kikubwa ni kuwa mbunifu na kuongeza kidogo kidogo vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako hiyo, hata kama huna kipato kikubwa inawezekana, si lazima uweke vyote kwa pamoja, lakini kadri unavyojaaliwa unabadili cha zamani na unaweka kinachoendana na wakati wa sasa.

Utanunua pazia leo lakini siku nyingine kitu kingine na hii pia itasaidia nyumba yako kuonekana mpya kila siku.

Ni ukweli kuwa vitu vya nyumbani vinabadilika kila baada ya kipindi kifupi, zuria ulilonunua miaka mitano iliyopita, haliwezi kuendana na wakati huu.

DONDOO

Na Restuta James

## Zingatia haya unapowaza jiko la nje



KAMA huna fedha za kutosha na unahitaji jiko la nje wala usiwaze tena. Kuna njia za kuwa na sehemu ya kupikia yenye hadhi nzuri na mandhari ya kuvutia na kuifanya nyumba yako kuwa ya kisasa kila wakati.

Mtaalamu wa bustani Georgia Lindsay, ameandika kwenye mtandao wa Houzz kuwa jiko la nje linaweza kuwekwa kwenye eneo la bustani kwa kuweka karo la kuoshea vyombo, vyakula na jiko lenyewe. Hii ni aina ya ubunifu ambao unawapa nafasi wenye nyumba kufurahia mazingira ya nje badala ya kila siku kutumia ndani pekee.

Katika eneo hili la jiko, wanafamilia wanaweza kufurahia mlo hapo hapo nje kwa kuandaa mazingira yaani kuweka meza na viti au mkeka kwa wanaopenda kukaa chini.

Mtaalamu mwingine wa bustani, Anna Elias, anasema jiko la aina hiyo linaweza kuongezewa thamani kwa kuweka 'vibenchi' vya watoto ambavyo wanaweza kuvitumia kuchora na kupaka rangi aina mbalimbali ya kazi wanazoandaa.

"Jiko hili linapendeza kama kutakuwa na maua au miti ili kuondoa hali ya jiko la ndani. Pia unaweza kuezeka ili uweze kulitumia wakati wa mvua au jua kali. Ni zuri sana pale ambapo unaalika marafiki au ndugu kwa chakula cha mchana au usiku," anasema.

Anna anasema jiko hilo linawawezesha wageni na wenyeji kufurahia mlo kwa kuona jinsi unavyoandaliwa na pengine watu wanaweza kuonja wakati wa kupika hadi chakula kinaiva.

"Katika jiko hili mnaweza kujikuta familia nzima mnapika, ni eneo zuri sana," anasema.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
MIFUKO IKIBUMA INAFANYA BAR KUSIENDEKE, BASI KILA KIPINDI NITAKIONA KIZURI
'KARA-GOSI'
JUKWAANI
NATAKA KUWAONYESHA WANAOSEMA BIA IMENITAWALA WAJUE MIMI NDIO NIME-ITAWALA
'MALIMWENGU!'
MIEZI MITATU YA UKURUGENZI NIMEPIGA BILIONI TATU UNUSU WALIPONISHTUKIA NIMEISUSA AKAUNTI NA HIZO HELA ZOTE! HADI MSHAHARA NIMEUTELEKEZA HA HA HAAA!
WEWE HUJAIBA BALI 'UMEHOMOLA' HA HA HAAAAA KWA KUSUSA HELA UTAFIKA MBINGUNI NA VILAKA HA HAAA!
KUNA JAMAA KANAMBIA AKIFANIKIWA ATATOA MAALI MILIONI TATU. SASA WEWE UTATOA NGAPI KUMPIKU ILI NIKAPINDUE MEZA UMUOE WEWE YULE MCHUMBA?
WEWE NI MSHENGA AU DALALI? TUTAMBUANE
MTANI USITEGEMEE KITONGA NIMECHUNGULIA NIMEONA KAZI UNAYO
WEWE UME-CHUNGULIA, MIMI NIME-ANGALIA NIME-ONA SHIDA IKO PALEPALE UNAKUFA SABA KESH!!!!

# Baraza la mpito kuongoza Haiti

**PORT AU PRINCE,** HAITI

HATIMAYE baraza la utawala la mpito limeundwa nchini Haiti, lenye jukumu la kujaza pengo la uongozi na kurejesha hali ya utulivu.

Nchi hiyo haina serikali kwa sasa baada ya waziri mkuu Hariel Henry kujiuzulu baada ya magenge ya kihalifu wanaomiliki silaha kuendelea kufanya ghasia.

Tangazo la kuundwa kwa baraza hilo lilitolewa Ijumaa kupitia gazeti rasmi la "Le Moniteur", mwezi mmoja baada ya Henry kuachia madaraka.

Tangazo hilo, ambalo lilicheleweshwa kwa wiki kadhaa kutokana na mizozo ya kisiasa, limeleta matumaini katika juhudi za kupelekwa kikosi cha polisi cha kimataifa kilichoidhinishwa na Umoja wa Mataifa, kikiongozwa na Kenya.

Kutokana na hatua hiyo, baraza hilo lina jukumu la kuteua waziri mkuu mpya na serikali haraka ikijumuisha watu wenye mirengo mbalimbali ya kisiasa nchini humo.

Kuundwa kwa baraza hilo linaloungwa mkono na Marekani pia ni hatua ya kwanza kuelekea kufanyika uchaguzi wa rais ifikapo mwaka 2026.

Hata hivyo, maswali bado yamesalia ikiwa serikali ya mpito, iliyopewa jina la Baraza la Mpito la Rais, itaweza kuwa na nguvu dhidi ya magenge ya kihalifu yanayodhibiti sehemu kubwa ya mji mkuu Port-au-Prince.

Sehemu ya maelezo ya taarifa hiyo ilieleza kwamba baraza la mpito litatumia mamlaka mahususi ya urais wakati wa kipindi chote cha mpito hadi uchaguzi wa rais ambao lazima ufanyike kabla ya Februari 7, 2026.

Nchi hiyo haijafanya uchaguzi tangu 2016 na imekuwa bila rais tangu Jovenel Moise alipouawa 2021.

Waziri Mkuu Henry alishindwa kuingia nchini mwake baada ya kuwa na ziara Kenya, mwezi Februari, akijaribu kuandaa kikosi cha polisi cha kimataifa wa kulinda amani.

Baada ya shinikizo kali kutoka Marekani na nchi za kikanda, Henry alikubali kujiuzulu na kuwezesha kuundwa kwa baraza la mpito.

Ghasia hizo zimesababisha wafungwa wapatao 4,000 kuachiliwa baada ya magenge kuvamia magereza mawili makubwa na kushambulia na kuvunja milango.

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto UNICEF, lilionya kuwa tatizo la njaa na utapiamlo vinaendelea kushuhudiwa nchini humo.

**DW**



Raia wa Haiti wakipita mbele ya Ikulu ya rais iliyoko katika mji mkuu wa Port-au-Prince,

# Watu saba wauawa Goma baada ya kuvamiwa na waasi

**GOMA,** DRC

WATU saba wameuawa katika Hifadhi ya Virunga iliyoko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) baada ya waasi kuwavamia wakati wakiandaa nishati ya mkaa.

Taarifa kutoka eneo la Goma, ilisema hali imezidi kuwa mbaya kutokana na kukumbwa na mashambulizi ya waasi wa M23.

Kulingana na wakazi wa eneo hilo, waasi wa M23 wamekataza watu wa maeneo wanayodhibiti kwenda katika Hifadhi ya Virunga kwa misingi kwamba wanaweza kuchanganyikiwa kutokana na wanamgambo wengine kuwa na ngome.

Watu wote waliokufa wanatoka katika kijiji cha Karambi, katika eneo la Rushuru, kilomita thelathini kaskazini mwa mji mkuu wa mkoa wa Kivu Kaskazini wa Goma.

"Tuligundua kwamba walikuwa wamefungwa kamba na kuuawa," alisema mkazi mmoja wakati alipohojiwa na shirika la habari la AFP kwa njia ya simu.

"Waliuawa kwa mapanga siku ya Jumatano, miili yao ilipatikana juzi," alisema ofisa wa eneo hilo.

Alisema wayu hao wanaume walikuwa na umri wa kati ya miaka 20 na 30.

Kulingana na afisa huyo, watu wanaingia katika msitu huo kutokana na kukosa njia nyingine za kujikimu.

Wahusika wa mauaji hayo bado hawajatambuliwa, lakini wakazi hao wanashutumu M23, ambao wanasaidiwa na vitengo vya jeshi la Rwanda kuhusika na tukio hilo.

Katika kusaidia kupambana na waasi hao, jeshi la DRClilitoa wito kwa makundi yenye silaha yanayojulikana kwa jina la wazalendo kuingia katika mapigano.

Hifadhi ya Virunga ni kongwe zaidi ya asili barani Afrika, iliyoundwa mnamo 1925, inasifika kuwa wanyamapori mbalimbali kama sokwe wa milimani.

**RFI**

# Marekani yaiomba Iran kuacha kulipiza kisasi

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, amesema kwamba anatarajia Iran itafanya shambulizi la kulipa kisasi hivi karibuni.

Tishio hilo linalochukuliwa kuwa la kuaminika linaiweka Marekani katika kipindi kigumu na kumfanya kiongozi huyo kuitaka Irani kujizuia kuishambulia Israel.

"Usifanye hivyo, sitaki kutoa taarifa za siri, lakini natarajia kutokea hivi karibuni. Tumejitolea kwa ulinzi wa Israeli. Tutaiunga mkono Israel. Tutaisaidia Israel kujilinda na Iran haitafanikiwa," alisema Joe Biden akiitolea wito Iran kwa kifupi.

Alisema Ikulu ya White House inaona kuwa taarifa za kijasusi ilizozipata kwenye shambulizi lililokuwa likikaribia la Iran ni za kuaminika.

Aidha, maofisa wa Marekani walikataa kueleza kwa undani zaidi taarifa za kijasusi walizonazo, lakini Mshauri wa Mawasiliano wa Usalama wa Kitaifa John Kirby, aliona tishio hilo kuwa la kweli na linaonekana.

Hata hivyo, ofisa mkuu wa kijeshi wa Marekani katika Mashariki ya Kati aliwasili nchini Israel.

Maofisa wa Wizara ya Ulinzi ya nchi hiyo walisema bila maelezo zaidi, kwamba jeshi la Marekani katika eneo hilo limeimarishwa.

Siku moja baada ya shambulio la Israel lililofanyika katika mji wa Damascus nchini Syria, Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, alieleza kuwa nchi yake iliwajibisha Marekani ambaye ni mshirika wa Israel. Kwa upande wake, Israel imeonekana kuogopa majibu ya Tehran na linasumbua sehemu ya raia wa nchi hiyo. Baadhi ya raia wa Israel walieleza kuwa hawahisi kama wanalindwa na serikali yao. Tangu Oktoba 7, kumekuwa na hofu ya ukosefu wa usalama nchini humo ingawa wengi wanadhani hawawezi kushindwa.

MAKALA

# SI KILA USHAURI UNA NIA NJEMA



Na Magabilo Masambu

Kuna ndoa nyingi zimevunjika kwa sababu ya ushauri wa watu wa pembeni. Wengine wanatumia uzoefu wa matatizo yao kuwa matatizo yako, furaha zao kuwa zako na uhusiano wao kuwa wako. Jambo la msingi hapa ni kutambua kwamba kuna baadhi ya mambo ni ya kipekee hayafananishwi na mengine.

Ni kweli kwamba kila mtu ameumbwa na vipawa mbalimbali, hivyo anaweza kuwa anafahamu mambo mengi kutokana na uwezo huo. Pamoja na vipawa hivyo, hawezi kuwa anaelewa kila kitu kwa sababu atakuwa na uwezo wa kuelewa katika maeneo pekee aliyobarikiwa nayo.

Tofauti ya binadamu na wanyama wengine kama mbuzi, kondoo, punda na ng'ombe ni kitu kinachoitwa utashi. Utashi ni uwezo wa kutambua baya na jema. Baya na jema likifanyika uwe na uwezo wa kutambua na kuchukua hatua katika njia sahihi, kulipokea au kulikataa.

Nakubali kwamba wako watu wanaoyaona mambo kwa usahihi kabla ya kutokea na kuona wanalo jukumu la kutoa ushauri yasifanyike au yafanyike kwa namna ambayo wanafikiri yatazuia mambo fulani mabaya kutokea.

Upande wa pili pia wako wanaoyaona mambo mazuri yakiwa mbele, lakini kwa makusudi wanachukua hatua ya kutoa ushauri ili yale mazuri yasitokee.

Unaweza kupewa ushauri wa kisiasa, kielimu au kijamii. Ushauri kwa asili yake huwa hauzingatii taaluma ya mtu. Unaweza kupewa na ushauri na mtu yeyote na kazi itakayokuwa mbele yako ni kupokea au kuukataa. Kitendo cha kuchagua kama umeupokea au umeukataa, kinategemea uwezo wako wa fikra na utashi katika yale uliyoshauriwa.

Ukiwa na uwezo mdogo wa fikra dhidi ya aliyekushauri juu ya jambo fulani, kuna hatari ya ama kukataa ushauri mzuri au kukubali ushauri mbaya.

Ushauri wowote huwa hauhitaji sana majadiliano, bali tafakuri ya ndani kabisa kabla hujachukua uamuzi ya kuukataa ama kuukubali.

Kuna ndoa nyingi zimevunjika kwa sababu ya ushauri wa watu wa pembeni. Wengine wanatumia uzoefu wa matatizo yao kuwa matatizo yako, furaha zao kuwa zako na uhusiano wao kuwa wako. Jambo la msingi hapa ni kutambua kwamba kuna baadhi ya mambo ni ya kipekee hayafananishwi na mengine.

Katika siasa, ushauri umesababisha matatizo makubwa sana duniani hasa katika Afrika. Wako watu wameumizwa vibaya kwa sababu ya ushauri unaotokana na watu wengine. Kuna wengine wanafikiri nchi zao zilivyo ndivyo nchi zingine zilivyo pia.

Mwenyezi Mungu alikuwa na makusudi ya kuifanya Amerika iwe tofauti na Uingereza au Tanzania kuwa tofauti na Rwanda na kadhalika.

Maana yake ni kwamba kinachofanyika Amerika kitakuwa tofauti na kinachofanyika Uingereza. Pia kinachofanyika Tanzania lazima kiwe tofauti na kinachofanyika Uganda, hivyo yatakuwa makosa makubwa kuchukua uzoefu wa Zambia kuiendesha Malawi. Tafsiri yake ni kwamba Rais wa Zambia akipewa ushauri wa namna ya kuiendesha nchi yake kutoka Botswana, lazima achuje kwa kutumia utashi wake juu ya jambo gani alitekeleze au aliache.

Eneo la elimu pia limeathirika zaidi na ushauri wa watu. Leo hii kuna wazazi wakimwona jirani yao ameanza kazi fulani na baada ya mwaka mmoja kajenga nyumba na anamiliki gari, lazima wamshauri kijana wao akasome alichosomea jirani huyo bila kufahamu kwamba inawezekana kipato chake hakitokani tu na ujira wake.

Wako watu ambao wamesoma kozi fulani na baadaye kugundua kwamba walikosea kuchagua. Wako waliokosea kwa sababu walichagua kwa kutojua na kwa kutoshauriwa japo wengine walikosea kwa kushauriwa na watu wao wa karibu lakini baadaye wakabadilisha.

Tukubali ushauri wa watu lakini kabla ya kuutekeleza unahitajika umakini, tahadhari lakini tafakuri ya kutosha.Tukipokea kama ambavyo dodoki linanyonya maji kwenye bakuli, basi kama si leo ni kesho tutakuwa tunajutia uamuzi wa ushauri wenyewe.

Wakati mwingie tunatekeleza ushauri wa maadui wa wale wanaotushauri.

Hatuna sababu ya kubeba maadui wa watu wengine kwa mwavuli wa ushauri kwa sababu Rais wa Kwanza wa Tanzania. Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema: "Mtu yeyote mwenye akili, akikushauri jambo la kipumbavu na anajua unajua ni jambo la kipumbavu, ukilikubali atakudharau."

Kuna wengine wanakushauri ili wapate cha kukusema nacho baadaye. Ubaya wa ushauri mambo yakiharibika washauri huwa hawajitokezi kusema sisi ndio tulimshauri badala yake husema tulijua tu mambo yataharibika. Lakini matokeo yakiwa mazuri, watajitokeza na kusema alifanyia kazi ushauri wetu.

Kwa hiyo ni muhimu kuwa makini sana na kila aina ya ushauri unaopewa kwa sababu si kila ushauri una manufaa kwako. Wengine wanatafuta kujipendekeza ili kutimiza haja ya mioyo yao kutoka kwako maana wanajua wewe ndiwe unaweza kutimiza ndoto zao.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *'Nakupenda, lakini baba yangu kavunjika mguu kwa ajili yako'*



Na Adam Fungamwango

Kitu hicho kilisababisha wambea waanze kujua kuna namna kati yao, kwa sababu pamoja na kijana kuonekama yupo peke yake, lakini ni mgeni kijijini hapo, hivyo wakawa wanafuatilia nyendo zake. Habari zikamfikia baba wa msichana. Na akaonyeshwa kijana huyo wa kijiji cha jirani, lakini sasa alikuwa anaonekana kushinda kijijini Nsobombo. Hakumwambia binti yake. Aliacha kwanza, nadhani alikuwa na mipango yake.

Ni kisa cha kusisimua na kusikitisha sana. Kinahusiana na mambo ya mapenzi. Mapenzi yana vitu vingi sana ambavyo kama wasanii wetu wa sasa wangeendelea kuchambua kama walivyofanya wanamuziki wa huko nyuma, tungepata mikasa na visa vingi sana, lakini pia jamii kujifunza mengi.

Bahati mbaya sana wao wanaishia 'nakupenda' na maneno yenye ukakasi, ambayo wakati mwingine huwezi kukaa hata na familia yako ukasikiliza, achilia mbali wat unaowaheshimu mno kama baba au mama mkwe.

Kisa hiki kilitokea kweli miaka mingi nyuma katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, maeneo ya Kamina, kwenye kijiji cha Nsobombo, alikozaliwa mwanamuziki, Tshimanga Kalala Asossa. Kijana mmoja wa vijiji vya jirani alikutana na msichana kutoka Nsobombo, wakaongea waliyoongea na kukubaliana kuwa wapenzi.

Hata hivyo, kila mmoja aliendelea kuishi kwao, badala yake walikuta wanakokujua wenyewe na kuongea mambo yao.

Msichana mara kwa mara alikuwa akimsitizia jamaa kuwa hata siku moja asijaribu kufika nyumbani kwao kumfuata, au kumuulizia kwa sababu baba yake ni mkali, na si utamaduni wa Mwafrika.

Dada wa watu akamwambia asubiri kwanza, ataanza mwenyewe kujieleza kwa wazazi kama amepata mchumba, halafu jambo likishakaa vizuri, basi atamwita kwenda kujitambulisha rasmi akiwa na mshenga pamoja na barua ya posa mkononi. Wakakubaliana hivyo.

Mapenzi yao yakaendelea kwa kificho tu. Tatizo ni kwamba kijana akaanza kuwa na wivu kupindukia. Kijijini kwao hakukaliki, kiguu na njia kwenda Nsobombo kwa mpenzi wake.

Kitu hicho kilisababisha wambea waanze kujua kuna namna kati yao, kwa sababu pamoja na kijana kuonekana yupo peke yake, lakini ni mgeni kijijini hapo, hivyo wakawa wanafuatilia nyendo zake. Habari zikamfikia baba wa msichana. Na akaonyeshwa kijana huyo wa kijiji cha jirani, lakini sasa alikuwa anaonekana kushinda kijijini Nsobombo. Hakumwambia binti yake. Aliacha kwanza, nadhani alikuwa na mipango yake.

Siku isiyo na jina, kijana akapita maeneo ya nyumbani kwa msichana. Alipopita akapunguza mwendo na kuanza kuangalia huku na huko kama anaweza kumwona mpenzi wake, lau kwa macho tu.

Mzee akamwona alivyokuwa wakishangaashangaa na alivyoambiwa, kuonyeshwa, aliunganisha doti na kuamini kuwa yule ndiye kijana anayemharibu binti yake. Akatoka mbio ndani na panga na kuanza kumkimbiza jamaa.

Kijana akatoka mbio na kwa sababu umri bado alimchengesha mzee, mwishoni alianguka shimoni na kuvunjika mguu. Mzee akalazwa hospitalini.

Ikawa ni simulizi vijiji vyote vya jirani. Binti akakasirika na kumfuata mpenzi wake kijijini kwao, akakutana naye na kuanza kumlaumu kwa yote aliyoyafanya. Mwishoni akamwambia ni kweli anampenda lakini anavunja uhusiano kwa sababu hakufuata maagizo yake na haiwezekani kuendelea na mapenzi wakati baba yake anateseka hospitalini, pia hata kama akileta barua haitoweza kupokewa tena.

Asossa alikichukua kisa hiki na kukitungia wimbo aliouita 'Salimia', ikiwa ni jina la kijana huyo na ulirekodiwa na kwenye studio za Radio Tanzania Dar es Salaam mwanzoni mwa miaka ya 1990.

"Kufika kwako kwetu Salimia kumezua jambo, baba kavunjika mguu katumbukia shimoni alipokuwa anakukimbiza yoyoyo. Mpenzi nashindwa aaa, sijui niamue vipi, kukupenda bado kakupenda aaa, lakini baba yangu miye Nsobombo.

Mpenzi nashindwa aaa, sijui niamue vipi, kukupenda bado kakupenda aaa, lakini baba yangu miye Nsobombo.

"Kufika kwako kwetu Salimia kumezua jambo, baba kavunjika mguu katumbukia shimoni alipokuwa anakukimbiza yoyoyo.

Mpenzi nashindwa aaa, sijui niamue vipi, kukupenda bado kakupenda aaa, lakini baba yangu miye Nsobombo.

"Mpenzi nashindwa aaa, sijui niamue vipi, kukupenda bado kakupenda aaa, lakini baba yangu miye Nsobombo. Yoyoyo ona sasa mpenzi Salimia, haraka yako mpenzi, mimi sasa naumia, baba hospitalini anateseka, wewe upate mapenzi, yananisumbua, nifanye sasa nini eee, Salimia baba.

"Angalia kukosa kwa imani yako kwangu, nilikwambia usifike nyumbani kwanza, niachie mwenyewe Salimia, nikajieleze kwa wazazi wangu, hukutaka kunisikia Salimia, matokeo yake baba kabaki kilema. Mimi na wewe Salimia naona basi tena

Angalia kukosa kwa imani yako kwangu, nilikwambia usifike nyumbani kwanza, niachie mwenyewe Salimia, nikajieleze kwa wazazi wangu, hukutaka kunisikia Salimia, matokeo yake baba kabaki kilema. Mimi na wewe Salimia naona basi tena."

Hivi wasanii wa kike hapa nchini wanashindwa kweli kutunga nyimbo kama hizi ambazo za mikasa ya mapenzi, badala yake wanaishia kuimba maneno yasiyofaa?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba aliyomwelekeza aende kumuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, saa chache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HERI akasogea pembeni tena ya kitanda na kujaribu kukokota kile ambacho kipo uvunguni, na lengo ni kumtoa panya aliyekufa ambaye anatoa harufu kali.

Kilichotoka sasa ni mtego wa panya. Lakini haukuwa mzima. Ulikuwa ni mtego wa zamani ambao uliharibika. Tangu uharibike hajanunua mtego mwingine. Ulikuwa umeshaanza kuwa na kutu, ukiwa hauna uwezo wa kukamata hata mende, achilia mbali panya, kwa sababu waya na vitu vingine ambayo vinasababisha uitwe mtego vimeshaharibika.

Hapo akachoka zaidi. Akaachana na alichokuwa anafanya, akakaa chini.

Dakika mbili baadaye akasimama na kuzunguka chumba kizima, akitafuta kitu kile kile na sehemu zile zile ambazo ameshapita. Hakuna kilichobadilika.

Alipoangalia saa yake kwenye simu yake ya kitochi ilimwambia imebaki nusu saa tu mgeni awasili.

Wakati wenzake wanakuwa na furaha wanapokuwa na ahadi na wapenzi wao, yeye sasa alichukia.

Akatamani Nuru apate dharura yoyote ile asifike siku hiyo. Harufu iliendelea kuzidi na kuanza kumsumbua hata yeye mwenyewe. Akakaa kwenye kitanda kwanza ili atulize akili na kuona nini cha kufanya.

Mawazo yakamrudisha nyumba, siku ya kwanza alipokutana na Nuru.

Yalikuwa ni majira fulani hivi ya saa 10:00 jioni, akiwa kwenye duka moja akinunua sabuni aliyoipenda kuiogea.

Akamkuta msichana mmoja aliyeonekana kama anazozana na muuzaji.

"Kwanza nakudai, juzi ulichukua unga kila moja, ukaniambia nitakuletea baadaye, hadi leo hujaleta, leo unakuja tena, umesahau kama jana ulikopa, unakuja kununua mchele pesa yenyewe pungufu," Heri alimshuhudia muuza duka akimpasha yule dada.

"Nitakuletea, shangazi bado anaumwa..."

"Hakuna, shangazi yako mwenyewe ana madeni kibao hapa, hajalipa, na wewe unakuja kumsaidia kuongeza madeni."

"Aiii Mangi, hatukudhulumu, shangazi akipona madeni yote yatalipwa."

"Yaani hadi apone? Hii ni biashara bwana. Asipopona je!? Unafikiri wakiwa sita kama yeye, mimi tena nitaweza kwenda mjini kununua bidhaa?"




Pamoja na kwamba alisimama dukani kwa muda mfupi tu wa sekunde kadhaa, lakini yale maongezi aliyaelewa vizuri sana.

Ni kwamba msichana yule anaishi kwa shangazi yake. Ambaye ana madeni kwenye duka hilo.

Kwa sasa Shangazi yake anaumwa, inaonekana kuna matatizo ya kipato, hivyo juzi alikuja kununua unga ili wakasonge ugali wake. Leo hii amekuja kununua mchele. Kwanza pesa yake haitoshi, pili anadaiwa.

"Naomba nisaidie sabuni." Akakatisha mzozo wao.

Muuzaji dukani ambaye kwa mujibu wa yule msichana anaitwa Mangi aliposikia sauti hiyo aliacha kuongea ghafla na kugeuka kumtazama Heri.

Sura yake iliyokuwa imeonekana kuchukia, ilibadilika ghafla na kutabasamu. Heri alimshangaa kwani hakujua kilichomfanya atoke kwenye hali ya kuchukia na kutabasamu.

"Watanzania bwana, ndiyo maana mkienda nchi jirani hampewi kitu. Wewe una pesa yako utasemaji, naomba nisaidie?" Maneno hayo yalimfanya ajue ni sasa ni kitu gani kinachozungumziwa.

**"Sasa kumbe, we una hela wako mfukoni, halafu useme, 'naomba, nisaidie', kweli. Wenzetu hiyo kwao si sawa, ila sisi Watanzania ni waungwana, hata kama kuna pesa yako na unanunua, lakini bado unatumia uungwana." Muuza duka akafafanua.**

"Yaani inaonekana kama tunaomba, si ndiyo?" Akachagiza kama vile ameelewa, lakini bado akahitaji ufafanuzi.

"Sasa kumbe, we una hela wako mfukoni, halafu useme, 'naomba, nisaidie', kweli. Wenzetu hiyo kwao si sawa, ila sisi Watanzania ni waungwana, hata kama kuna pesa yako na unanunua, lakini bado unatumia uungwana." Muuza duka akafafanua.

Wakati wanapiga stori za Wabongo na uungwana wao, yule binti bado aliendelea kusimama dukani.

Ni kwa sababu tayari mwenye duka alikuwa ameshikilia pesa yake mkononi.

Muda huo huo ambao alikuwa anatafuta sabuni, akamwambia mteja wake wa awali.

"Hii elfu mbili sikurudishii, nakata ilee ya juzi uliochukua unga, haya nenda kalete ya mchele."

"Mangi, sina hela nyingine leo tutalala na njaa wenzako..."

"Kwani vipi? Mbona tangu nakuja uko na huyu binti kama mnabishana hivi?"

Akaelezwa jinsi ilivyokuwa. Msichana hakusema lolote. Alibaki kimya.

Heri akaingiza mfukoni na kutoa noti ya shilingi elfu tano.

"Sasa sikiliza, hiyo uliochukua kata ya unga wa juzi, halafu hii sasa, mpimie mchele kilo ambacho alikuwa anahitaji..."

"Alikuwa anataka kilo moja," akadakiwa Mangi.

"Enhee, sasa chenji inayobaki mpe mwenyewe, inaweza ikakusaidia tena kesho."

Mangi alifanya kazi yake kama alivyoagizwa. Chenji iliyobaki alikabidhiwa msichana. Akaipokea.

Kitendo cha kuipokea kilionekana kumfariji sana Heri. Kwa muda mfupi tu aliyomuona hapo dukani alionekana kumpenda.

Ni msichana alionekana ana uzuri ulioyojificha. Umbile zuri, na urembo uliofichwa na kukosa matunzo nadhani pamoja na ugumu wa maisha anayopitia.

Hata yeye Heri hakuwa na pesa kiasi hicho, ni mbangaizaji tu wa kuuza viatu na mitumba ya kutandika chini, lakini vitu viwili vilimfanya kuitoa shilingi elfu tano.

Kwanza ni huruma kwa jinsi alivyokuwa akiomba, pamoja na historia ndogo tu aliyoisikia hapo na akashikwa na huruma.

Pili ni umbile ya msichana huyo lilimshtua. Licha ya kuonyesha hakuwa na maisha bora, hatas nguo tu alizokuwa amevaa, lakini aliweza kuwazidi hata wale wasichana wanaoshinda saluni.

Hilo halikuonekana sana kwenye machi ya kawaida. Ilibidi mtu mwenye jicho la tatu kuweza kutambua kuwa iwapo atatunzwa vyema, atakuwa mrembo mara kumi ya alivyo.

"Ahsante kaka." Heri alishtuliwa na shukrani kutoka kwa binti huyo.

"Usijali dada yangu. Unaitwa nani?"

"Naitwa Nuru.", akaitikiwa kwa sauti tulivu na ya upole. "Mhh! Na kweli Nuru." Akasema Heri na kusababisha binti wa watu kutabasamu.

Tayari Heri na Nuru walishaanza kuvuta hatua kadhaa kutoka dukani na sasa walikuwa wanatembea wakiwa wawili.

"Unaishi wapi?" Heri akauliza tena

"Hapa hapa Chanika, wala siyo mbali, nyumba hizo za nyuma hapo."

"Unaishi na nani?" Bado maswali yalikuwa yanafululiza kutoka kwa Heri.

"Shangazi," akajibu. Heri hakutaka kumwambia chochote kwa jinsi alivyotokea kumpenda mara tu baada ya kumuona. Alichoona ni kwamba muda wa kumwambia hivyo haijafika.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# DRAKE ANUSURIKA KIFUNGO



MAHAKAMA imemwachia huru mwanamuziki maarufu wa hip hop nchini Marekani, Drake, baada ya kumuona hana hatia katika kesi inayohusu tamasha la Astroworld 2021 lililofanyika Houston ambalo lilisababisha watu 10 kufa kwa kukosa hewa.

Katika tamasha hilo, Drake alikuwa mgeni maalumu wa msanii mwenzake Travis Scott, ambaye aliandaa onyesho hilo.

Mwishoni mwa tamasha hilo lililofanyika Novemba 5, umati wa watu ulipoongezeka katika eneo la tukio na kusababisha hali ya mkanyagano uliofanya wengi kuathiriwa kwa kukosa hewa.

Ilidaiwa mamlaka ya eneo hilo na waandaaji wa tamasha walijaribu kukatisha tamasha hilo, lakini haikusaidia kwani maafa yalizidi na kufanya watu 10 kufa papo hapo kwa kukosa hewa.

Walishtakiwa ikiwamo Drake na Scott, walimwomba Jaji wa mahakama hiyo ya Wilaya, Kristen Hawkins kufuta kesi dhidi yao na ombi hili lilikubaliwa kwa upande wa Drake na kutakiwa kuondoka mahakamani hapo.



## *AIC Nira, Lemi George wazidi kupaa*

MWIMBAJI wa muziki wa Injili jijini Mwanza, Lemi George na kwaya ya AIC Nira, wamefanikiwa kujizolea umaarufu kutokana na wimbo wao mpya 'Msalabani' kufanya vizuri katika majukwaa mbalimbali nchini.

Akizungumza na NIPASHE jana, Lemi, alisema anamshukuru Mungu kwa mapokezi mazuri ya wimbo huo ambao umefanya vizuri katika msimu wa Sikukuu ya Pasaka.

"Huu ni upendo mkubwa ambao mashabiki wa muziki wa Injili wametuonyesha mimi na AIC Nira Gospel Choir, video tayari ipo kwenye chaneli yetu yao ya YouTube na bado tunaomba watuunge mkono ili tuweze kuwafikia watu wengi zaidi," amesema Lemi.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PAQUETA ATAJWA CITY
KLABU ya Manchester City inaweza kutumia vyema nia ya Lucas Paqueta ya kuondoka West Ham msimu ujao - lakini iwapo tu uchunguzi wa FA kuhusu madai ya ukiukaji wa kanuni za kamari uliofanywa kwa kiungo huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 26 utatupiliwa mbali. (**Guardian**)

### MUSIALA ANUKIA CITY
MANCHESTER City ipo tayari kutumia pauni milioni 120 ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Jamal Musiala, mwenye umri wa miaka 21 kutoka Bayern Munich. (**TeamTalk**)

### EDWARDS KUTUA LIVERPOOL
LIVERPOOL inatayarisha uhamisho wa msimu wa majira ya joto kwa ajili ya mshambuliaji wa Sporting Lisbon, Marcus Edwards, mwenye umri wa miaka 25, na mlinzi wa Ureno, Goncalo Inacio (22). (**Football Insider**)

### ALMIRON, WILSON KUONDOKA
MSHAMBULIAJI wa Paraguay, Miguel Almiron, mwenye umri wa miaka 30 na mshambuliaji wa England, Callum Wilson (32), ni miongoni mwa wachezaji ambao wanaweza kuondoka Newcastle United huku klabu hiyo ikijiandaa kwa ujenzi wa majira ya joto. (**Telegraph**)

### ADARABIOYO KITAELEWEKA
MANCHESTER United na Tottenham Hotspur zimewasiliana na beki wa kati wa Fulham, Tosin Adarabioyo, katika kujaribu kufikia makubaliano ya awali ya mkataba mpya na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (**TeamTalk**)

### WAN-BISSAKA ANUKIA MILAN
AARON Wan-Bissaka wa United analengwa kwa pauni milioni 13 na Inter Milan huku beki huyo wa Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 26 akimalizika mkataba wake mwishoni mwa msimu wa 2025. (**Gazetta dello Sport**)

### GALLAGHER KUTUA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur inatumaini kukamilisha mkataba wa haraka kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 24, dirisha la uhamisho litakapofunguliwa. (**Sun**)

### BRENTFORD: TONEY HAUZWI
KOCHA wa Brentford, Thomas Frank, amepuuzia ripoti kuhusu mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuondoka kwa pauni milioni 30 msimu wa joto. (**Evening Standard**)

### GRIMALDO AGEOMBEWA ULAYA
ARSENAL na Liverpool zimeungana na Bayern Munich katika mbio za kuwania kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Hispania, Alejandro Grimaldo, mwenye umri wa miaka 28 kutoka Bayer Leverkusen. (**Express**)

### CUBARSI ANOGEWA BARCELONA
MLINZI wa Barcelona, Pau Cubarsi, anataka kusaini mkataba mpya huko Nou Camp licha ya klabu kubwa zote barani Ulaya kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17. (**Mundo Deportivo**)

### BARKLEY KUTOA MSIMAMO
KIUNGO wa kati wa Luton Town, Ross Barkley, amesema hatazingatia mustakabali wake hadi mwisho wa msimu huu, huku kukiwa na nia ya Manchester United. (**Express**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: CITY INA SHIDA KUBWA

**Ni kutokana na majeruhi alionao pamoja na uchovu wa...**

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amekiri timu yake imechoka, akisema wako kwenye "shida kubwa, kubwa, kubwa" kutokana na orodha yao ya sasa ya majeruhi.

Huku klabu hiyo ikiwinda kwa mara ya pili mfululizo kutwaa mataji makubwa, kiungo wa City, Rodri, aliomba kupumzika baada ya sare ya 3-3 dhidi ya Real Madrid katika mchezo wa mkondo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya uliochezwa Jumanne iliyopita.

"Angalia michezo yetu na utagundua," alisema Guardiola katika mkutano wake na waandishi wa habari kuhusu maoni ya Rodri.

"Ni rahisi. Yeye ni muhimu sana kwa ubora anaotupa. Lakini ikiwa una mchezaji ambaye hataki kucheza, hatacheza.

"Nahitaji kupuzisha sehemu za kati pia lakini katika michezo ya kirafiki ya England, John Stones na Kyle Walker walipata majeraha. Tuko katika matatizo makubwa.

"Nilihisi tulikuwa tumechoka katika mechi zilizopita. Tutaamua kesho kile tunachopaswa kufanya," aliongeza.

Guardiola hakuweza kutoa taarifa kuhusu utimamu wa Nathan Aké, Phil Foden na Walker.

Foden alilazimika kutoka nje kwa sare dhidi ya Madrid, huku Ake na Walker wakiwa tayari nje ya uwanja kutokana na majeraha.

"Tunafanya mazoezi na tutajua wanavyojisikia," alisema.

Mshambuliaji wa City, Erling Haaland, anaongoza katika orodha ya wafungaji mabao kwenye Ligi Kuu England akiwa na magoli 19, na Guardiola aliulizwa ni nini zaidi mfungaji wake mahiri anahitaji kufanya ili kushinda Ballon d'Or msimu huu baada ya kumaliza kama mshindi wa pili kwa Lionel Messi tuzo za mwaka jana.

"Anahitaji kucheza dakika zaidi, ili kujifunza kutokana na kile unachotakiwa kufanya," alisema Guardiola.

Nafasi ya 18 kwa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Kenilworth Road mwezi Desemba, lakini ikatoa timu hiyo inayosuasua kutoka Kombe la FA kwa kucharazwa 6-2 katika raundi ya tano mwezi Februari.

## HABARI MICHEZO



# DE JONG AHUSISHWA TENA KUTIMKA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

SAKATA lisiloisha juu ya mustakabali wa Frenkie de Jong wa Barcelona halionyeshi dalili ya kupungua, huku ripoti nchini Hispania zikimhusisha tena kiungo huyo kuhamia Paris Saint-Germain.

Mholanzi huyo alidokezwa kwa mara ya kwanza kuondoka katika klabu hiyo wakati wa dirisha dogo la usajili la 2022, wakati Manchester United ilipotaka kumfanya mchezaji wa kwanza kusajiliwa chini ya kocha mpya kwa wakati huo, Erik ten Hag.

Lakini baada ya miezi kadhaa ya uvumi, dhana na mazungumzo kati ya pande hizo mbili, Mashetani Wekundu hatimaye waliachana na harakati zao na kuamua kumsajili Casemiro kutoka Real Madrid kama mbadala wake.

Barcelona ilikuwa chini ya shinikizo kubwa la kuwauza wachezaji ili kushughulikia hali yao ya kifedha inayozidi kuwa mbaya, na hakuna mabadiliko mengi katika miaka miwili iliyofuata.

Miamba hao wa Katalunya bado wana deni kubwa, na Camp Nou kwa sasa inafanyiwa ukarabati wa euro bilioni 1.5, na bado wako katika shinikizo la kuwaondoa wachezaji wanaolipwa mishahara minono ili kufuata sheria za matumizi ya LaLiga.

De Jong amekuwa akieleza mara kwa mara nia yake ya kubakia Barcelona, ambayo bado yeye ni mchezaji wake muhimu, lakini vyombo vya habari vya Hispania vimefichua anaweza kuondoka kidogo kipindi cha majira ya joto kijacho.

PSG wanajiandaa kumpoteza Kylian Mbappe atakayejiunga na Real Madrid msimu huu - hatua nyingine ambayo imechukuliwa kwa muda mrefu - na kuondoka kwake kunakokaribia kuashiria mabadiliko katika sera ya uhamisho ya klabu.

De Jong amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake Barcelona, ikimaanisha ana uwezekano thamani yake kupanda msimu huu wa joto, na kwa sababu hiyo anasalia kuwa mmoja wa mali zinazowaniwa zaidi katika klabu hiyo.

Raphinha na Lamine Yamal pia wamehusishwa na kuondoka kwa fedha nyingi, ingawa wote wana majukumu muhimu ya kikosi cha kwanza.

# Kocha acheka bei ya Toney

**LONDON,** England

KOCHA mkuu wa Brentford, Thomas Frank amepuuza mapendekezo ya klabu hiyo kukubali ofa za pauni milioni 30 kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji wao, Ivan Toney.

Mshambulizi huyo wa England, Toney anatarajiwa kuondoka msimu huu wa joto huku mkataba wake ukimalizika mwaka 2025, na Frank tayari amekiri kuwa klabu hiyo itakuwa tayari kufanya biashara kwa bei inayofaa.

90min hivi karibuni iliripoti kwamba Arsenal imepunguza nia yao ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ingawa anaweza kuibuka kama chaguo kwa Manchester United katika harakati zao za kutafuta mshambuliaji mpya wa kati.

Chelsea pia wamekuwa wakihusishwa naye kwa kiasi kikubwa.


Ripoti kutoka Ujerumani mapema wiki hii zilisema Brentford ingefikiria kumuuza Toney kwa pauni milioni 30, lakini Frank ameamua kuingilia kati kuzungumzia suala la bei.

"Kwa kawaida siingii kwenye mambo ya bei, lakini ningesema hiyo ni nafuu sana kwa mfungaji mabao 20 kwenye Ligi Kuu," alisema katika mkutano na waandishi wa habari.

Rekodi ya mauzo ya Brentford ni pauni milioni 33 kutoka kwa Aston Villa kwa Ollie Watkins, ambaye alifunga mabao mawili dhidi yao wiki iliyopita katika sare ya 3-3.

David Raya atajiunga na Arsenal kwa ada ya kudumu ya pauni milioni 27 msimu huu wa joto baada ya washikabunduki kulipa pauni milioni 3 kama sehemu ya makubaliano yao ya awali ya mkopo.

Toney alirejea baada ya kufungiwa kwa miezi nane kwa kukiuka sheria za kamari Januari na tangu wakati huo amefunga mabao manne katika mechi 13 za Ligi Kuu ya England, huku akifunga bao lake la kwanza kwa England katika sare ya 2-2 na Ubelgiji wakati mapumziko ya mechi za kirafiki za kimataifa



Machi.

Baada ya kutolewa kwenye benchi kwa sare ya Jumamosi iliyopita dhidi ya Villa kutokana na jeraha dogo, Frank amethibitisha kuwa Toney yuko fiti.

"Kila mtu kutoka wiki iliyopita tulipokabiliana na Villa anapatikana," Frank aliongeza.

# Rodrygo anaweza kuivaa Man City

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti hatarajii kuwa bila Rodrygo kwa muda mrefu baada ya fowadi huyo wa Real Madrid kukosa mazoezi kutokana na jeraha.

Rodrygo alifunga na kuonyesha kiwango bora kwenye sare ya 3-3 ya Madrid na Manchester City, lakini akakosa mazoezi juzi, na kuwaacha mashabiki wakitoa jasho kutokana na kupatikana kwake kwa mechi ya marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itakayochezwa Jumatano.



Alipoulizwa kuhusu Rodrygo, Ancelotti alithibitisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anaweza kuwa tayari kwa mchezo huo.

"Rodrygo alipata maumivu, lakini atapatikana kama kikosi kizima," alisema Ancelotti.

"Kipaumbele ni yeye kucheza. Wiki hii tuko hatarini sana, lakini kama timu zote. Tunadumisha imani ya siku chache zilizopita."

Ancelotti alikiri kunaweza kuwa na mwanzo wa kwanza wa msimu kwa beki wa kati Eder Militao ambaye atarudi uwanjani baada ya kuwa nje ya dimba kwa miezi nane kwa kuumia goti.

"Narudia nilichosema: wote wanapatikana na nitaweka timu bora," aliongeza Ancelotti. Militao pia atapatikana.

"Nikiona mchezaji mwenye afya njema, sifikirii kuhusu dakika ambazo ametumia au muda aliokusanya mazoezini. Nilimchezesha Sami Khedira, ambaye alikuwa akitoka kwenye majeruhi katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na nilifanya hivyo kwa sababu niliona yuko mzima kwa wakati huo."

HABARI MICHEZO

# COASTAL UNION YAONGEZA 'JOTO' KWA SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mashujaa FC, umeifanya Coastal Union kujiwekea katika mazingira mazuri ya kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Ushindi huo wa Coastal Union pia unaweza kuzipa 'homa' vigogo vya soka nchini, Simba na Yanga pamoja na Azam FC zote za Dar es Salaam.

Mabao ya Shedrack Malungwe na Bakari Selemani yaliifanya Coastal Union ifikishe pointi 33, ikijikita katika nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikitangaza hali ya hatari kwa vinara Yanga, Simba na Azam, ambapo kama zitasuasua inaweza kutwaa moja kati ya nafasi tatu za juu walizozishikilia.

Mabingwa hao wa Tanzania Bara mwaka 1988, walikuwa vibonde katika mzunguko wa kwanza, walibadilika ghafla mzunguko wa pili ulipoanza kutokana na kufanya usajili mzuri kipindi cha dirisha dogo pamoja na kumwajiri Kocha Mkenya, David Ouma.

Mashujaa FC, ambayo iliiondoa Simba kwenye Kombe la FA, Jumanne iliyopita kwa mikwaju 6-5 ya penalti, baada ya sare ya bao 1-1, ilishindwa kabisa kukabiliana na vijana machachari wa Ouma.

Endapo itashinda mechi zake nane zilizosalia, Coastal Union itafikisha pointi 67, hivyo timu za Yanga, Simba na Azam kama zinataka kushikilia nafasi hizo tatu za juu, inabidi nazo zishinde mechi zao, ili kuepuka kuenguliwa.

Coastal Union imebakiza mechi za nyumbani dhidi ya Prisons (Mei 8, mwaka huu), Singida Fountain Gate (Mei 20), JKT Tanzania (Mei 27) na KMC (Mei 30), huku za ugenini zikiwa ni dhidi ya Namungo, (Aprili 17), Yanga (April 27), Geita Gold (Mei 15) na Kagera Sugar (Mei 21).

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa mabingwa watetezi, Yanga kucheza dhidi ya Singida Fountain Gate wakati Namungo watawakaribisha Azam FC kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi.




Mshambuliaji wa Mtibwa Sugar, Jimmyson Mwanuke (aliyeruka juu), akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Geita Gold FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Nyankumbu jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Viwanja kujengwa wilayani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema itajenga viwanja vya soka katika kila wilaya ili kurejesha hamasa ya mchezo huo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa Kamati ya Saidia Zanzibar Ishinde ambayo ni maalumu kwa timu zote za taifa za visiwani hapa.

Waziri huyo alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekusudia kuhakikisha sekta ya michezo inawekewa mazingira mazuri ikiwamo kupatikana kwa viwanja katika kila wilaya kwa sababu mpira wa miguu unachangia kwa kiasi kikubwa kutoa ajira kwa vijana.

"Tunataka kuhakikisha sekta hii inaendelea kuwa muhimu kwa vijana kupata ajira kutokana na kujituma zaidi katika kucheza soka, tumeona vijana wetu wengi wanacheza soka nje ya Zanzibar," alisema Mwita.

Naye Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed, alisema watabuni njia na mbinu ambazo zitaisaidia Zanzibar kufikia malengo yake hasa katika mashindano ambayo Zanzibar itashiriki.

"Tunatakiwa kuwa na mipango imara, mipango ambayo itasaidia kutimiza malengo ya kamati hii kwa timu zote za taifa kufanya vyema," alisema.

Aliongeza kwa mwaka huu kamati hiyo inajukumu la kuhamasisha timu yake kufanya vyema katika mashindano ya Kombe la Chalenji ambayo Zanzibar ni mwenyeji wa michuano hiyo.

## Sare ya nyumbani yawakera Prisons

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Prisons, Hamad Ally, amesema timu yake ilikosa ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC kutokana na wapinzani wao kucheza mfumo wa 'kupaki basi', ambao walifanikiwa.

Hamad alisema mfumo uliochezwa na timu hizo mbili kwenye Uwanja wa CCM Sokoine, Mbeya na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1, alisema licha ya kwamba kipindi cha kwanza.

"Sare haikuwa malengo yetu, tulipoteza umakini kipindi cha kwanza tukaruhusu bao, kipindi cha pili tulitawala lakini wapinzani wetu wakapata bao la kusawazisha dakika za mwishoni, mechi hii tulikuwa na uwezo wa kushinda, ila wenzetu kipindi cha pili waliingia na mfumo wa 'kupaki basi' na kutupa ugumu sana," alisema kocha huyo.

Maneno hayo yaliungwa mkono wa Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moallin, ambaye alisema waliamua kufanya hivyo kwa sababu wazidiwa hasa kipindi cha pili.

Matokeo ya mechi hiyo, yanaifanya Prisons kufikisha pointi 29, ikiwa nafasi ya tano katika msimamo wa Ligi Kuu huku KMC ikiwa nafasi ya sita na pointi kama hizo, lakini uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa unawabeba 'Wajelajela'.

## Kipanga bado yaota ubingwa wa Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BENCHI la ufundi la Kipanga FC limesema malengo yao kwa sasa ni kumaliza katika nafasi nne za juu baada ya kupoteza matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Hata hivyo Kocha Mkuu wa Kipanga, Hassan Abdulrahman, alisema hawajitoi moja kwa moja katika mbio za ubingwa kwa sababu huenda bahati ikawaangukia wao kutokana na matokeo ya wapinzani ingawa ushindani katika ligi hiyo umeongezeka.

Alisema ushindani na ugumu uliopo katika ligi hiyo unatokana na kila timu kupambana kujikwamua katika kipindi hiki cha lala salama.

Alisema timu yake itacheza mechi mbili za kirafiki ili kujiweka sawa kukabiliana na ligi hiyo itakayorejea tena kuanzia Aprili 27, mwaka huu.

"Tupo katika mbio za ubingwa ingawa tuna asilimia chache katika mbio hizo, lakini pia tunaangazia kuwa katika nafasi nne za juu, hili tunamatumaini makubwa," alisema kocha huyo ambaye timu yake iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo ikiwa na pointi 31.

# Michezo

Jumapili Aprili 14, 2024
Nipashe



De Jong ahusishwa tena kutimka Barca UK. 22



Mshambuliaji wa Simba, Fred Michael (jezi nyekundu), akiwania mpira dhidi ya beki wa kati wa Ihefu, Benjamin Tanimu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA YAPUNGUZWA KASI MBIO UBINGWA

## ●●● Bao la penalti lainusuru na kichapo cha nne mfululizo...

**Na Adam Fungamwango**

MASHABIKI wa Wekundu wa Msimbazi walilazimika kusubiri dakika nane kabla ya mechi kumalizika ili kushuhudia timu yao ikipata bao la kusawazisha dhidi ya Ihefu SC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida jana.

Alikuwa ni Clatous Chama aliyefunga kwa penalti dakika ya 82 na kuifanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya bao 1-1, huku yeye mwenyewe akifikisha magoli saba mpaka sasa kwenye orodha ya wafungaji wa ligi hiyo msimu huu.

**Kabla ya hapo, mashabiki wa timu hiyo walikuwa wamekaa 'roho juu' tangu dakika ya 41 ambapo wenyeji Ihefu walipopata bao la kuongoza.**

Zilikuwa ni juhudi binafsi za Kibu Denis, aliyekuwa nyota wa mchezo wa jana kwa upande wa Simba, aliyeangushwa ndani ya eneo la hatari na beki wa kati wa Ihefu, Mukrim Issa, na mwamuzi kuamuru adhabu hiyo ambayo ilibadilisha ubao wa matokeo.

Bao hilo liliinusuru Simba kupata kipigo cha nne mfululizo, kwa sababu ilifungwa mara mbili na Al Ahly ya Misri, nyumbani bao 1-0 na ugenini mabao 2-0 katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kabla ya kuondoshwa tena katika michuano ya Kombe la FA kwa kuchapwa penalti 6-5 dhidi ya Mashujaa FC, Jumanne iliyopita.

Matokeo ya jana yanaifanya Simba kuongeza pointi moja na kufikisha 46, ikibaki pale pale katika nafasi ya tatu ya msimamo wa ligi, ikifikisha mechi 20.

Sare hiyo, imeipandisha Ihefu kutoka nafasi ya 11 hadi ya tisa ikiwa na pointi 24 kibindoni.

Mchezo ulianza kwa Ihefu kuonekana hawana wasiwasi, badala yake walikuwa wakigongeana pasi fupi fupi na ndefu kiasi cha dakika moja kupita bila wachezaji wa Simba kuugusa mpira.

Dakika ya nne Simba ilifika langoni kwa Ihefu kwa mara ya kwanza na kukosa bao la wazi kupitia straika wake, Fredy Michael, aliyeupata mpira nje ya eneo la hatari akiwa peke yake, akaingia nao ndani, lakini alitumia muda mrefu kufikiria kupiga hadi alipofika hatua nne toka kwa kipa, Aboubakar Khomeny, kabla ya beki Benson Mangolo, kuufagia.

Dakika moja baadaye Ihefu ilijibu shambulizi hilo kupitia kwa straika wake, Elvis Rupia, aliyewachachafya mno mabeki wa Simba jana, baada ya kuunganisha moja kwa moja krosi ya Morice Chukwu, lakini mpira ukapaa juu ya lango.

Simba iliendelea kukosa mabao ya wazi, dakika ya tano kupitia kwa Freddy tena, na dakika ya 20, alipomiminiwa krosi na Chama, lakini baada ya kuuweka mpira wavuni, akamchezea madhambi, Khomeny.

Sadio Kanoute naye pia alikosa bao dakika ya 21, baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Saido Ntibazonkiza ya kumwekea pasi ya nyuma, ambapo alipiga shuti kubwa lililopita juu ya lango la Ihefu.

Shuti la kwanza la Ihefu lililolenga lango ndiyo lililozaa bao dakika ya 41, lililowekwa wavuni na Duke Abuya aliyeitendea haki krosi ya Mkenya mwenzake, Rupia.

Lilikuwa ni kosa la kipa wa Simba, Ally Salim kuufuata mpira huo wa krosi, lakini akaukosa, ukamkuta Duke ambaye alimwacha akiwa ameanguka chini, akamlamba chenga beki, Fondoh Cha Malone na kuujaza wavuni kirahisi.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko kadhaa ambayo yaliongeza spidi ya mpira, Luis Miquissone wa Simba kama angekuwa na bahati angeipatia timu yake mabao mawili, dakika ya 78, alipiga shuti kali akiwa ndani ya eneo la hatari ambalo Khomeny alilipangua na dakika mbili kabla ya mechi kumalizika, shuti lake lilioonekana kwenda wavuni, liliwababatiza mabeki wa Ihefu na kupaa juu kidogo ya lango.

Baada ya mechi hii, Simba inakwenda kujiandaa kuwakabili watani zao wa jadi, Yanga, mechi itakayochezwa Aprili 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Yanga, Singida FG hesabu uwanjani

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanahitaji kuvuna pointi tatu muhimu katika mchezo wa ligi hiyo dhidi ya wenyeji Singida Fountain Gate FC utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Yanga inahitaji ushindi ili kuendelea kujiimarisha kileleni katika vita ya kuwania taji la Ligi Kuu wakati wapinzani wao wanataka kuvuna pointi tatu ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema amekiandaa vyema kikosi chake na wachezaji wote wapo tayari kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu na si jambo lingine.

Gamondi alisema licha ya kukosa maandalizi mazuri kuelekea mchezo wa leo kwa sababu ya kutumia muda mrefu safarini baada ya kumaliza mchezo uliopita, bado anaamini nyota wake watapambana ili kupata ushindi.

"Nawaheshimu Singida Fountain Gate, tumefanya maandalizi mazuri na ya msingi, muhimu ni kushinda mechi ya kesho (leo) ili kuendelea kusalia katika uongozi wetu wa ligi hiyo," alisema Gamondi.

Naye Kocha Msaidizi wa Singida Fountain Gate FC, Ngawina Ngawina, alisema wanacheza na timu kubwa na kwa kuzingatia hilo wamefanya maandalizi bora kuhakikisha wanaibana Yanga ndani ya dakika 90.

Ngawina alisema wachezaji wake wana hali nzuri wamejipanga kuhakikisha wanaishangaza Yanga katika mchezo huo.

" Tunahitaji pointi tatu, tunafahamu ubora wa Yanga, tutacheza kwa tahadhari kubwa ili kufikia malengo yetu katika mchezo huu. Kwa misimu hii miwili Yanga iko vizuri kila mmoja analifahamu hilo, hatuwaogopi, tunawaheshimuna," alisema Ngawina.

Nyota wa Singida Fountain Gate, Habib Kyombo, alisema benchi la ufundi limemaliza jukumu lao na kazi iliyobaki ni kwao wachezaji kwenda kuonyesha mchezo mzuri ili kupata matokeo chanya.

"Tuko tayari kupambana, safu yetu ya ushambuliaji iko vizuri, mchezo wa kesho (leo), utakuwa mzuri kwa sababu mwalimu ameandaa timu na mbinu, tunajua nini tunaenda kufanya katika mchezo huo dhidi ya Yanga," alisema Kyombo.

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042